UTT AMIS
Asset Management and Investor Services

KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS

# TAARIFA YA MWAKA YA MFUKO WA UWEKEZAJI WA HATIFUNGANI (BOND FUND)

BOND FUND
More ideas for your money

## KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2024

# YALIYOMO


1. Ratiba na Ajenda za Mkutano ........ ii
2. Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Nne ........ 1
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Nne ........ 24
4. Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi ........ 27
5. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko wa Hatifungani ........ 31
6. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko ........ 33
7. Taarifa ya Hesabu za Mfuko ........ 36
8. Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji ........ 41
9. Jarida la Habari ........ 48


BOND FUND
More ideas for your money

**KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS**
**MKUTANO MKUU WA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA HATIFUNGANI**
**SIKU YA JUMAPILI TAREHE 17 NOVEMBA 2024 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE – DAR ES SALAAM**

# RATIBA NA AJENDA ZA MKUTANO

| MTIRIRIKO WA SHUGHULI | | | |
|---|---|---|---|
| **S/N** | **MUDA** | **SHUGHULI** | **WAHUSIKA** |
| 1. | 02.30 - 02.45 | Kuwasili kwa Wajumbe na Kujiorodhesha | Wajumbe/Utawala |
| 2. | 02.45 - 03.00 | Matangazo na Shughuli za Utawala | MC/Utawala |
| 3. | 03.00 - 03.05 | Kuthibitisha Akidi na Kufungua Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |
| 4. | 03.05 - 03.20 | Utambulisho (Wakurugenzi, Menejimenti na Watoa Huduma wa Mfuko) | Mkurugenzi Mtendaji |
| 5. | 03.20 - 03.30 | Kupitia Muhtasari Kutoka Kwenye Mkutano Wa Nne | Wote |
| 6. | 03.30 - 03.45 | Kupitia Taarifa Za Yatokanayo Kutoka Kwenye Mkutano Wa Nne | Mkurugenzi Mtendaji |
| 7. | 03.45 - 04.00 | Taarifa ya Mwenyekiti | Mwenyekiti wa Bodi |
| 8. | 04.00 - 04.30 | Kupokelewa kwa Taarifa ya Mwaka<br>1. Mwangalizi wa Mfuko<br>2. Mkaguzi wa Hesabu<br>3. Taarifa ya Hesabu | <br>CRdB<br>KpMg<br>Mkurugenzi wa Fedha na Mipango |
| 9. | 04.30 - 05.00 | Kupokea Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji | Mkurugenzi wa Uwekezaji |
| 10. | 05.00 - 05.35 | Kipindi cha Maswali na Majibu | Bodi/Menejimenti |
| 11. | 05.35 - 05.45 | Kufunga Mkutano | Mwenyekiti Wa Bodi |

# 2 Muhtasari wa Mkutano wa Nne (4 ) wa Mwaka

## WALIOHUDHURIA (Kiambatisho "A")

### BODI YA WAKURUGENZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Casmir S. Kyuki | - | Mwenyekiti wa Bodi |
| 2. | Dkt. Judika L. King'ori | - | Mkurugenzi wa Bodi |
| 3. | Bw. David E. Mwankenja | - | Mkurugenzi wa Bodi |
| 4. | Bw. Paul A. Maganga | - | Mkurugenzi wa Bodi |
| 5. | Bi. Neema Jones | - | Mkuruenzi wa Bodi |
| 6. | Bw. Simon M. Migangala | - | Mkurugenzi Mtendaji |

### WAJUMBE WA KAMATI ZA BODI YA WAKURUGENZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Dkt. F. Magambo | - | Mjumbe wa Kamati ya Bodi |
| 2. | Bw. L. Kakulu | - | Mjumbe wa Kamati ya Bodi |
| 3. | Bw. D. Olesumayan | - | Mjumbe wa Kamati ya Bodi |

### WAALIKWA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Vicent Wanjala | - | KPMG / Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko |
| 2. | Bi. Rashidah Rashid | - | KPMG / Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko |
| 3. | Bi. Z. Yusuph | - | CRDB / Waangalizi wa Mfuko |
| 4. | Bi. H. Mushi | - | CRDB / Waangalizi wa Mfuko |
| 5. | Bi. L. Kondo | - | CRDB / Waangalizi wa Mfuko |
| 6. | Bw. E. Nambala | - | CRDB / Waangalizi wa Mfuko |
| 7. | Bi. Anna Gabriel | - | CMSA / Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana |
| 8. | Bi. Mariam Mtunguja | - | CMSA / Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana |
| 9. | Bw. Josephat Masaba | - | Mwakilishi wa Msajili wa Hazina |

### MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. S. Migangala | 27. | Bi. P. Kasilati |
| 2. | Bw. I. Wahichinenda | 28. | Bi. S. Kapufi |
| 3. | Bi. J. Msofe | 29. | Bw. C. Josiah |
| 4. | Bw. D. Mbaga | 30. | Bw. M. Mchanjila |
| 5. | Bw. S. Kaniki | 31. | Bw. J. Mwangomola |
| 6. | Bi. P. Nchimbi | 32. | Bi. M. Minja |
| 7. | Bw. S. Bujiku | 33. | Bi. J. Mlimbila |
| 8. | Bi. S. Mgaya | 34. | Bw. M. Balati |
| 9. | Bi. T. Mpiluka | 35. | Bw. H. Mnongane |
| 10. | Bi. J. Swai | 36. | Bw. B. Liwali |
| 11. | Bw. D. Balima | 37. | Bw. C. Chanjarika |
| 12. | Bw. R. Mwanga | 38. | Bw. J. Joseph |
| 13. | Bw. M. Kimario | 39. | Bi. R. Maruma |
| 14. | Bw. P. Ndunguru | 40. | Bw. J. Masoud |
| 15. | Bi. V. Abuogo | 41. | Bi. E. Simon |
| 16. | Bw. F. Bwalya | 42. | Bw. A. Mushi |
| 17. | Bw. B. John | 43. | Bw. F.Lushinge |
| 18. | Bw. W. Khijja | 44. | Bw. B.Lukinga |
| 19. | Bi. W. Malya | 45. | Bi. M.Mashiku |
| 20. | Bi. A. Laurent | 46. | Bi.V. Mashindano |
| 21. | Bw. S. Khatibu | 47. | Bw. A. Kandila |
| 22. | Bw. S. Rugaitika | 48. | Bi. L. Malimiru |
| 23. | Bw. A. Ambari | 49. | Bi. H. Lashikoni |
| 24. | Bw. J. Nyambo | 50. | Bi. D. Milenge |
| 25. | Bi. W. Makumbati | 51. | Bi. J. Njovu |
| 26. | Bi. V. Maheri | | |

## 1.0 AKIDI NA KUFUNGUA MKUTANO

Mwenyekiti alifungua mkutano saa 8:26 Mchana kwa kuwakaribisha wajumbe walioweza kuhudhuria Mkutano wa 4 wa Mfuko wa Hatifungani. Kabla ya ufunguzi wa kikao, wajumbe walisomewa taarifa ya akidi, ambayo ilionyesha kwamba Wajumbe wenye Vipande waliohudhuria walikuwa 1,145 ambao majina yao yameambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi kama Kiambatisho "A". Mkurugenzi Mtendaji alitoa taarifa kwamba idadi ya Vipande vilivyowakilishwa ni 534,255,302.967 kati ya jumla ya Vipande 4,842,253,364.369 vya Mfuko. Taarifa ilitolewa kwamba idadi ya Vipande vilivyowakilishwa ni asilimia 11% ya jumla ya Vipande vyote vya Mfuko na hivyo Mkutano ungeweza kuanza kwa sababu akidi inayohitajika kwenye Waraka wa Makubaliano (Deed of Trust) ni asilimia 10.

## 2.0 DONDOO ZA MKUTANO

Wajumbe walikubaliana na dondoo/ajenda zifuatazo:

1. Akidi na Kufungua Mkutano
2. Kupitisha Dondoo/Ajenda za Mkutano
3. Utambulisho
4. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
5. Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
6. Taarifa ya Mwenyekiti
7. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko
8. Taarifa ya Mkaguzi wa Mfuko
9. Taarifa ya Hesabu za Mfuko
10. Taarifa ya Meneja wa Mfuko Kuhusu Uwekezaji
11. Kipindi cha Maswali na Majibu
12. Kufunga Mkutano

## 3.0 UTAMBULISHO

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwatambulisha Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya UTT AMIS, Wajumbe wa kamati za Bodi na Wawakilishi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Pia aliendelea kuwatambulisha Mwakilishi wa Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko, Wawakilishi wa Kampuni ya KPMG inayotoa Huduma za Ukaguzi wa Heesabu za Mfuko pamoja na Mwakilishi kutoka ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo inasimamia Taasisi za serikali. Mkurugenzi Mtendaji alimalizia kwa kutambulisha Menejimenti ya UTT AMIS Pamoja na wafanyakazi wote waliokuwepo Mkutanoni kwa ujumla.

## 4.0 KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

Baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa kumbukumbu za Mkutano wa tatu (3) uliofanyika tarehe 20 Novemba 2022, Wajumbe wote walipitisha na kuuthibitisha kama kumbukumbu rasmi za Mkutano huo.

## 5.0 YATOKANAYO NA MUHTASARI WA MKUTANO ULIOPOITA

### 5:1 Namna ya uwasiliashaji taarifa za hesabu za mfuko

Ili taarifa ya Hesabu ieleweke zaidi kwa wawekezaji, ilielezwa kwamba maelezo zaidi yatakuwa yanatolewa wakati wa uwasilishaji wa Taarifa.

## 6.0 TAARIFA YA MWENYEKITI

6.1 Mwenyekiti aliwasilisha taarifa ya Mfuko wa Hatifungani kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2023.Taarifa hiyo ilieleza kwamba katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 30, 2023, utendaji wa mfuko ulikuwa mzuri. Faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa ikilinganishwa na Kigezo Linganifu.(Performance Benchmark) . Faida kwa mwaka ilikuwa asilimia 12.3 ikilinganishwa na asilimia 9.7 ya Kigezo Linganifu. Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2023, thamani ya mfuko iliongezeka kutoka shilingi billioni 219.8 iliyofikiwa tarehe 30 Juni 2022 hadi Shilingi billioni 423.6 tarehe 30 Juni 2023. Ongezeko hili la thamani ya Mfuko linatokana na imani ya wawekezaji pamoja na kueleweka kwa elimu inayotolewa kuhusu faida za mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

6.2 Ilielezwa kwamba wakati Dunia inazidi kupata ahueni juu ya athari za UVIKO 19 na madhara ya vita vya Ukraine pamoja na uchumi, taarifa kwa mujibu wa machapisho ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, pato la taifa (Gross Domestic Product) lilikua kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022 na kiwango cha asilimia 5.4 katika kipindi cha robo mwaka ya kwanza na ya pili ya mwaka 2023. Ukuaji uchumi wa Tanzania umekuwa ni zaidi ya ukuaji katika nchi za ukanda wa Jangwa la Sahara na nchi za ukanda wa Ushirikiano wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambao ni asilimia 3.5. Kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu ya Tanzania, kipindi cha robo mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni,2023, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.0, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 12.6 kwa nchi za Afrika Mashariki na asilimia 17.1 kwa nchi za ukanda wa SADC. Kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita, viwango vya riba katika soko havikubadilika sana, ikiashiria uimara wa soko kwa ujumla. Kwa upande mwingine, thamani ya

Shilingi ya Tanzania dhidi yad Dola ya Marekani ilipungua kidogo kwa kiwango cha asilimia 1.0 na kuongezeka thamani dhidi ya fedha za baadhi ya nchi za Afrika Mashariki kwa viwango vya hadi asilimia15.0

6.3 Kuhusu maendeleo ya Soko la Mitaji na Dhamana, ambalo utendaji wake hupimwa kwa kuangalia mabadiliko ya Fahirisi(Tanzania Share Index), imeonesha kuwa na maendeleo mazuri. Katika kipindi cha mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni 2023, kumekuwa na ongezeko la asilimia 4.1 ambapo iliongezeka toka 3,928.5 tarehe 30 Juni 2022 hadi 4,091.8 tarehe 30 Juni 2023. Ongezeko hilo ni chini ya lile la tarehe 30 Juni 2022 ambalo lilikuwa ni asilimia 7.5. hii inamaanisha kuwa, kwa kipindi cha mwaka ulioshia tarehe 30 Juni 2023, bei za Hisa kwa ujumla ziliongezeka japo kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na mwaka uliopita. Sababu za kupanda kwa bei za Hisa kulichagizwa na utendaji mzuri wa Kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, kuongezeka imani kwa wawekezaji wa ndani na wan nje ya nchi na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Tunamshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kusimamia na kuweka mazingira bora ya biashara.

6.4 Kuhusu utendaji wa Mifuko, Mwenyekiti alieleza kwamba, kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2023, viashiria vya kiuchumi vinaonyesha kwamba Kampuni ya UTT AMIS pamoja na mifuko inayoisimamia inaendelea kufanya vizuri. Thamani ya Mifuko imeongezeka kutoka Shilingi billioni 996.5 tarehe 30 June 2022 hadi kufikia Shilingi trilioni 1.535 tarehe 30 Juni 2023. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 54.0 ambapo ni sawa na Shilingi 538.9 ikilinganishwa na ongezeko la Shilingi 383.7 sawa na asilimia 62.6 kwa mwaka uliotangulia. Ongezeko hili, limeenda sambamba na ongezeko la idadi ya wawekezaji 29,832 sawa na asilimia 17.0 waliojiunga katika mwaka wa fedha uliotangulia. Faida kwa Mfuko wa Hati Fungani kwa mwaka unaoishia Juni 2023 ilikuwa asilimia 12.3.

6.5 Mwenyekiti aliendelea kutoa taarifa kuwa UTT AMIS inaendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka mitano unaoishia Juni 2024 kwa kuendelea kujikita kwenye matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji kwa njia ya mitandao. Katika miaka mitatu iliyopita Kampuni ya UTTAMIS ilizindua utoaji wa huduma kwa wawekezaji kwa kutumia simu za kiganjani na inaendelea na uunganishaji wa mifumo ya kibenki na mifumo ya UTT AMIS. Lengo kuu la uunganishwaji wa mifumo hii ni kuongeza ufanisi kwa kupunguza mlolongo wa hatua za uchakataji wa miamala inayofanywa kwa njia za kibenki. Kufuatia kukamilika uunganishwaji wa mifumo ya UTT AMIS na benki ya CRDB ambayo pia ni waangalizi wa Mifuko, Kampuni ya UTT AMIS pia imekamilisha kuunganisha na mifumo ya benki za NMB, NBC, na Benki ya Stanbic. Aidha, UTT AMIS imeendelea na miradi ya kuunganisha na mifumo ya Benki ya EXIM, Benki ya ABSA, Benki ya KCB, Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya DCB na Benki ya UBA ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Ni matumaini yangu kuwa pindi miradi hii itakapokamilika, miamala ya kidijitali, ambayo sasa ni asilimia 70 itaongezeka na kufikia asilimia ya juu zaidi. Kampuni ya UTT AMIS itaendelea kuelimisha umma juu ya manufaa ya matumizi ya njia za kidijitali katika utekelezaji huku ikiendelea kuwekeza katika mifumo mipya ili kutoa huduma bora zaidi kipindi kijacho.

6.6 Kuhusu Mafanikio kwa kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kampuni ya UTT AMIS unaoishia Juni 2024, Mwenyekiti alisema kumekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa. Ikiwa umebaki mwaka mmoja wa utekelezaji wa mpango mkakati huo, Kampuni imeshaanza kuandaa mpango mkakati wa wa kipindi cha 2024 mpaka 2029, utakao lenga, Pamoja na mambo mengine, kuboresha mifuko na huduma kwa wawekezaji pamoja na kubainisha fursa nyingine za kibiashara kwa manufaa ya wawekezaji, Serikali pamoja na wadau wengine. UTT AMIS itaendelea kuboresha uendeshaji wa mifuko ili uwe wa kisasa zaidi na kuhakikisha wawekezaji wanapata faida shindani na nzuri kuendana na hali ya soko.

6.7 Katika kuhitimisha taarifa yake, Mwenyekiti aliwashukuru wawekezaji wote kwa ushirikiano na Imani waliyonayo kwa UTT AMIS na Mfuko wa Hatifungani kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Kwa namna ya kipekee aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Mwangalizi wa Mfuko ambaye ni Benki ya CRDB, Soko la Hisa la Dar es Salaam na madalali wake, Wawekezaji, na wafanyakazi wa UTT AMIS na Wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha UTT AMIS kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha wa 2023. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utaendelea kwa manufaa ya Wawekezaji katika Mifuko na maendeleo ya Soko la Mitaji na Sekta ya Fedha hapa Nchini kwetu.

## 7.0 TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO

7.1 Mwakilishi wa Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko wa Hatifungani, aliwasilisha Taarifa iliyoeleza kwamba jukumu lao ni kusimamia na kuhakikisha kwamba utendaji wa Meneja wa Mfuko unazingatia Waraka wa Makubaliano ili kuhakikisha maslahi bora kwa wawekezaji.

7.2 Mwakilishi huyo alieleza kuwa katika utekelezaji wa kazi yao kama Mwangalizi wa Mfuko wana majukumu mbalimbali yakiwemo uangalizi wa mali za Mfuko, kuhakikisha Meneja wa Mfuko anatumia njia au mbinu sahihi katika kukokotoa mahesabu ya thamani ya Mfuko sambamba na Waraka wa Makubaliano, na pia kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa na kusaidiana na meneja wa mfuko katika kukusanya, kuwafikia wateja pamoja na kuwasaidia kuuza vipande vyao.

7.3 Mwakilishi wa Benki ya CRDB alisema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichoanza tarehe 01.07.2022 mpaka 30.07.2023. Benki ya CRDB kama Mwangalizi wa Mfuko wa Hatifungani imeendeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za Meneja wa Mfuko, utekelezaji wake na kuangalia changamoto kwenye uwekezaji.

7.4 Mwakilishi wa Benki ya CRDB alihitimisha kwa kuwathibitishia Wawekezaji wa Mfuko kwamba shughuli za uwekezaji kwenye Mfuko wa Hatifungani na kwa wajibu wa Meneja wa Mfuko vimeendeshwa na kutekelezwa kufuatana na vipengele vya Waraka wa Makubaliano na kwamba maslahi ya wenyevipande ndani ya Mfuko wa Hatifungani yanalindwa na kuzingatiwa ipasavyo, na Meneja ameendesha Mfuko kulingana na Waraka wa Makubaliano.

## 8.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MFUKO WA HATIFUNGANI

8.1 Mwakilishi kutoka Shirika la Wahasibu la KPMG ambao ni Wakaguzi wa Mfuko aliwasilisha muhtasari wa taarifa kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. ilielezwa kuwa taarifa ya Hesabu za Mfuko zilizowasilishwa yaani taarifa ya Mapato na Matumizi, taarifa ya Urari wa Hesabu za Mfuko, taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko na taarifa ya Mtiririko wa Fedha umetayarishwa kutoka katika taarifa kamili ya ukaguzi ya Mfuko wa Hatifungani kwa kipindi cha mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2023.

8.2 Mwakilishi huyo alieleza kuwa Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha hauoneshi taarifa zote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (International Financial Reporting Standards (IFRS)). Taarifa ya wakaguzi iliendelea kusema kwamba Muhtasari huo wa hesabu za kifedha siyo mbadala wa taarifa kamili ya hesabu za kifedha iliyokaguliwa. Pia ilielezwa kwamba Muhtasari wa hesabu za kifedha pamoja na taarifa kamili ya hesabu zilizokaguliwa haijumuishi matukio au miamala baada ya tarehe za taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa.

8.3 Pia mwakilishi huyo alieleza kwamba maoni ya ukaguzi (audit opinion) yasiyokuwa na kasoro juu ya taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha za Mfuko yalitolewa kwenye taarifa ya tarehe 11 Novemba, 2023 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Taarifa kamili ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023 inajumuisha mambo mengine muhimu juu ya ukaguzi wa hesabu za mfuko.

8.4 Mwakilishi huyo alihitimisha taarifa yake kwa kueleza kuwa majukumu yao kama wakaguzi wa hesabu za mfuko ni kutoa maoni kama muhtasari wa hesabu za Mfuko unaendana na taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha na kwa mujibu wa taratibu zao za ukaguzi, ukaguzi ambao ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standards on Auditing –ISA) 810 (kama ilivyorekebishwa), "Kazi za kuripoti juu ya Muhtasari wa taarifa za kifedha".

## 9.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU HESABU ZA MFUKO WA HATIFUNGANI

Mkurugenzi wa Huduma za Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Hesabu za Mfuko katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

9.1 Ilielezwa kuwa Taarifa ya hesabu za Mfuko wa Hatifungani, imegawanyika katika sehemu kuu nne, ambazo ni Taarifa ya Mapato na Matumizi (income statement), Taarifa ya Urari wa Hesabu za Mfuko (Financial Position), Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko (Statement of Changes in Net Assets Attributable to Unit Holders) na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha (Statement of Cash Flows).

9.2 Kwa upande wa Mapato na Matumizi, Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha mwaka ulioishia 30 Juni, 2023, jumla ya Mapato ya Mfuko yalikuwa Shilingi 48,351,089,000 /= ikilinganishwa na Shilingi 27,166,640,000/= kwa mwaka 2022. Mapato haya yanatokana na weledi wa meneja wa mfuko katika kuwekeza kwenye hati fungani za serikali. Pia ilielezwa kuwa jumla ya gharama za uendeshaji kwa mwaka ulioishia 30 Juni, 2023 ilikuwa Shilingi

8,823,531,000/= ikilinganishwa na Shilingi 4,318,978,000/= zilizotumika mwaka 2022, hivyo kufanya Mapato baada ya kutoa gharama za uendeshaji na kabla ya kodi kuwa Shilingi 39,527,558,000/= ikilinganishwa na Shilingi 22,487,662,000/= kwa mwaka wa 2022. Aidha Mfuko umeweza kulipa Gawio kwa wawekezaji kiasi cha Shilingi 34,749,875,000 /= kwa mwaka ulioishia Juni 2023 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 16,577,941,000/= kwa mwaka ulioishia Juni 2022. Kodi iliyotozwa na Serikali ilikuwa Shilingi 243,403,000/= kwa mwaka ulioishia Juni 2023 ikilinganishwa na Kiasi cha Shilingi 165,468,000/= kwa mwaka ulioishia Juni 2022 . Hivyo, Mfuko ulibaki na faida halisi (baada ya Kodi na Matumizi) ya Shilingi 4,534,280,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

9.3 Kwa upande wa Urari wa Hesabu za Mfuko, ilielezwa kuwa Rasilimali za Mfuko zilikuwa Shilingi 429,625,151,000/= mnamo tarehe 30 Juni, 2023, ikilinganishwa na Shilingi 222,028,416,000/= mnamo 30 Juni 2022. Dhima za Mfuko zilikuwa Shillingi 8,869,050,000/= mnamo tarehe 30 Juni, 2023 ikilinganishwa na Shilingi 3,337,419,000/= mnamo tarehe 30 Juni 2022. Hivyo thamani halisi ya Mfuko mnamo tarehe 30 Juni, 2023 ilikuwa Shilingi 420,756,101,000/= ikilinganishwa na Shilingi 218,690,997,000/= tarehe 30 Juni 2022.

9.4 Katika Taarifa ya Mabadiliko ya thamani ya Mfuko ilielezwa kuwa thamani ya mfuko mwanzoni mwa mwaka yaani Julai 1, 2023, ilikuwa shilingi 218,690,997,000/=ikilinganishwa na shilingi 92,751,982,000 mwaka 2022. Ongezeko kutokana na faida ya Mfuko ilikuwa Shillingi 4,534,280,000/= kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2023 ikilinganishwa na Shilingi 6,104,253,000/= mwaka ulioishia Juni 2022, miamala ya vipande (net sales) ilipatikana Shilingi 197,530,824,000/= ikilinganishwa na Shilingi 119,834,762,000/= ya mwaka ulioishia 30 Juni 2022. Hivyo Thamani halisi ya Mfuko tarehe 30 Juni 2023 ilikuwa Shilingi 420,756,101,000/= ikilinganishwa na Shilingi 218,690,997,000/= tarehe 30 Juni 2022.

9.5 Kwa upande wa Taarifa ya Mtiririko wa Fedha, ilielezwa kuwa fedha halisi iliyotokana na shughuli za uendeshaji kabla ya marekebisho ya mtaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023, zilitumika Shilingi 801,350,000/= ikilinganishwa na ongezeko la Shilingi 1,701,591,000/= kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2022. Aidha fedha halisi iliyotumika kwenye shughuli za Uendeshaji baada ya marekebisho ya mtaji na kodi ya Serikali ilikuwa Shilingi 165,051,267,000/= ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 111,219,193,000/= kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2022. Fedha/amana halisi kutoka kwenye vipande ilikuwa Shilingi 164,587,084,000/= kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2023 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 104,352,581,000/= zilizopatikana mwaka 2022. Salio la fedha mwanzoni mwa mwaka 2023 lilikuwa shilingi 2,407,031,000 ikilinganishwa na shilingi 9,273,643,000 mwanzoni mwa mwaka 2022 hivyo Mfuko kubaki na salio la fedha taslimu la Shilingi 1,942,848,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023 ikilinganishwa na salio la Shilingi 2,407,031,000/= mwishoni mwa mwaka 2022.

## 10.0 TAARIFA YA MENEJA WA MFUKO KUHUSU UWEKEZAJI

Mkurugenzi wa Idara ya Uwekezaji ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Meneja kuhusu uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

10.1 Taarifa ilieleza kuwa, Mfuko wa Hatifungani ulianzishwa mwezi septemba 2019 na hutoa fursa kwa wawekezaji kupata gawio, mwekezaji huchagua mojawapo kati ya aina tatu za mpango wa gawio (a) Gawio la kila mwezi (b) Gawio la kila nusu mwaka (c) Kukuza mtaji. Mahitaji ya awali ya uwekezaji ni shilingi elfu Hamsini(50,000/=) na kiwango cha nyongeza kisichopungua shilingi elfu tano (5,000/=) kwa wawekezaji wenye mpango wa kukuza mtaji tu. Mwekezaji anaruhusiwa kuchukua fedha zake wakati wowote anaohitaji na bila kutozwa gharama za kutolea [exit load], hivyo kudhihirisha kuwa mfuko wa Hatifungani ni fursa maridhawa kwa wawekezaji.

10.2 Taarifa hiyo iliainisha mgawanyo wa uwekezaji wa Mfuko wa Hatifungani ambapo ilieleza kuwa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS ilitumia uzoefu na weledi katika kufikia mgawanyo wa rasilimali kwenye uwekezaji wake wenye kuleta tija huku ikizingatia sera na miongozo mbalimbali inayotumiwa katika uwekezaji. Taarifa ilieleza kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 mgawanyo wa rasilimali za Mfuko ilikuwa kama ifuatavyo: asilimia 98.01 ziliwekezwa kwenye dhamana za serikali za muda mrefu, asilimia 1.98 ziliwekezwa katika amana za benki za muda maalumu na asilimia 0.01 katika amana na benki za muda mfupi. Hali ya utendaji wa mfuko ni nzuri na shindani ikilinganishwa na kigezo cha ufanisi na maeneo linganifu ambapo kwa mwaka 2023 faida ni asilimia 12.3 ikilinganishwa na asilimia 9.7. Mwasilishaji alieleza kwa kipindi hicho kiwango cha faida kilipungua kutoka asilimia 14.9 hadi asilimia 12.3. Aidha sababu ya kupungua ilielezwa kuwa ni kutokana na kupungua kwa viwango vya faida sokoni.

10.3 Taarifa iliendelea kueleza kwamba ni muhimu kufahamu kwamba Mfuko wa Hatifungani unaruhusu wanachama wake kuuza vipande vyao wakati wowote hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata fedha pindi anapozihitaji. Faida ya Mfuko inatolewa sawa kwa wawekezaji wote ikijumuisha wawekezaji wa kipato kidogo, wa kipato cha kati na wale wenye kipato kikubwa. Taarifa ilieleza kuwa viwango vya faida na ulinganifu kwenye maeneo mengine ya Uwekezaji.

10.4 Ilielezwa pia kwamba mwenendo wa uchumi wa Tanzania umekua stahimilivu na imara. Kwa mwaka 2022 uchumi ulikua kwa kiwango cha asilimia 4.7, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.9 mwaka 2021. Hata hivyo, kilimo,Ujenzi na Madini vilikuwa vichocheo vikubwa kwa ukuaji wa uchumi katika kipindi hicho. Uchumi kwa mwaka 2023 unakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 5.2, ukichagizwa na kufufuliwa kwa shughuli za kiuchumi hususani uwekezaji kwenye sekta ya umma na binafsi nchini. Pato la taifa hutafsiri kiwango na shughuli za uchumi katika nchi. Hali imara na stahimilivu juu ya mwenendo wa uchumi nchini ni muhimu kwa Mifuko ya uwekezezaji wa Pamoja inayosimamiwa na UTT AMIS na maeneo mengine ya uwekezaji nchini. Uchumi imara husaidia na kuimarisha thamani ya uwekezaji na huvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kwa upande wa Mfumuko wa bei nchini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 ni asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 4.4 iliyonakiliwa tarehe 30 Juni 2022. Kupungua kwa mfumuko wa bei nchini kunaashiria gharama za bidhaa na huduma mbalimbali zilipungua kwa mwaka ulioishia Juni 2023 ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo Juni 2022. Hivyo basi hali ya uchumi na mwenendo wa mfumuko wa bei ni stahimilivu kiasi ambacho kimewezesha wawekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji kuwekeza kwa wingi. UTT AMIS inajitahidi kuwekeza kwenye maeneo yanayotoa faida shindani kuliko kiwango cha mfumuko wa bei.

10.5 Kwa upande wa sekta ya benki, kwa kipindi cha mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni 2023, utendaji kwa sekta ya benki nchini imeendelea kuwa stahimilivu na yenye faida. Jumla ya rasilimali ziliongezeka kutoka shilingi trilioni 45.7 mwaka 2022 hadi shilingi trilioni 53.7 Juni 2023, ongezeko kwenye rasilimali ni shilingi trilioni 8.0, sawa na asilimia 17.5. Jumla ya amana kwenye benki iliongezeka kwa shilingi trilioni 5.7 sawa na asilimia 20.3 kutoka shilingi trilioni 28.0 Juni 2022 hadi shilingi trilioni 33.7 Juni 2023. Kwa upande wa mikopo imefikia shilingi trilioni 31.5, sawa na asilimia 21.6 ikilinganishwa na shilingi trilioni 25.9 mwaka uliopita. Ongezeko kwenye kiwango cha mikopo kilisababishwa na kupungua kwa masharti na viashiria vya hatari miongoni mwa wateja. Hata hivyo, viashiria vya hatari kwenye mikopo ya wateja wadogo na Taasisi zisizo za kifedha vilipungua ikilinganishwa na mwaka uliopita. Kuimarika kwa sekta ya benki ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na uchumi kwa ujumla kwani huduma zitolewazo na benki huchochea ufanisi kwenye uchumi. Aidha, hadi tarehe 30 Juni 2023 UTT AMIS imweza kuunganisha mifumo na benki ili kuwezesha wawekezaji kununua vipande kidigitali, hivyo kurahisisha uwekezaji mahali popote.

10.6 Mwasilishaji alieleza, namna sekta ya mawasiliano inavyoendelea kuchochea na kurahisisha uwekezaji katika mifuko na huduma binafsi. Taarifa iliainsha kuwa kwa kupiga *150*82# au kwa kutumia programu tumizi (UTTAMIS APP) mwekezaji anaweza kufungwa akaunti na kuona uwekezaji wake. Aidha kupitia simu mwekezaji anaweza kuuza na kununua vipande.

10.7 Taarifa ya meneja ilieleza kiasi cha Dhamana za Serikali za muda mrefu kwenye soko la awali ni shilingi trilioni 4.3 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.3 mwaka uliopita. Kiwango cha ushiriki kwenye minada hiyo kilipungua hadi shilingi trilioni 4.6 (asilimia 28.1) ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.8 mwaka uliopita. Aidha, kiwango kilichokubaliwa na Benki kuu ya Tanzania baada ya mnada kiliongezeka kwa shilingi trilioni 1.2 (asilimia 44.4) hadi shilingi trilioni 3.9. Kwa kipindi cha mwaka mmoja hali ya ushiriki wa wawekezaji kwenye dhamana za serikali za muda mrefu ilipungua ikilinganishwa na ongezeko la ushiriki kwenye dhamana za muda mfupi.

10.8 Faida katika dhamana za serikali za muda mfupi zilipungua kwa wastani wa asilimia 3.5 Juni 2023 kutoka asilimia 4.1 mwaka 2022. Ilielezwa kuwa viwango vya riba katika mkopo na faida katika amana vilivyongezeka ikilinganishwa na viwango vilivyonakiliwa mwaka 2022. Aidha viwango vya riba za mkopo katika benki za biashara ni asilimia 16.7 ikilinganishwa na asilimia 16.2 mwaka 2022. Uwekezaji katika amana za benki kwa muda wa mwaka mmoja zilitoa faida ya asilimia 8.2 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka uliopita.Viwango vya faida kwenye dhamana za serikali za muda mrefu havikubadilika tangu mabadiliko hayo yafanyike mwezi wanne mwaka 2022.

10.9 Taarifa ya meneja ilieleza kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja kilichoishia mwezi Juni 2023, viwango vya kubadilisha fedha kati ya Shilingi ya Tanzania na fedha za kigeni vimeendelea kuwa stahimilivu. Thamani ya Shilingi kwa Dola moja ya kimarekani ilikuwa imara na ya kuridhisha, ikisaidiwa na kuwepo kwa hali nzuri kwenye bei za bidhaa na huduma nchini, thamani ya fedha

nchini imebaki kuwa imara, ingawa ilipungua thamani kidogo dhidi ya Dola ya Marekani kwa asilimia 1.0 (Tsh 23.4) hadi Tsh 2,339.1 kutoka Tsh 2,315.7 iliyorekodiwa mwaka uliopita. Ilielezwa pia kwamba uimara wa viwango vya kubadilisha fedha ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na maeneo mengine ya uwekezaji kwa ujumla kwa sababu husaidia kutunza thamani ya rasilimali ambazo uwekezaji wake upo katika Shilingi ya Tanzania na kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya Tanzania.

10.10 Ilielezwa kuwa, kwa muda wa mwaka mmoja ulioishia mwezi Juni 2023 kumekuwa na viashiria chanya. Tuliona utoaji wa hatifungani mbili mpya za benki ya taifa ya biashara (NBC-Twiga) na benki ya biashara ya Kenya (KCB-Fursa Sukuk) zilizofanikiwa kufanya vizuri kwani jumla ya shilingi 49.9 zilipatikana. Pia mwezi Novemba 2022, Shirika la Watumishi Housing (WHI) lilizindua Mfuko wa uwekezaji wa Pamoja unaoitwa Faida (Mfuko wa Faida) ambao ulifanikiwa kuvutia wawekezaji na hadi Disemba mfuko ulinakili shilingi bilioni 7.9. Ushiriki katika soko la mtaji na dhamana kwa wawekezaji wa ndani na nje umeimarika kutokana na umma kupata uelewa kuhusu uwekezaji na matumizi ya mifumo ya kidigitali. Taarifa ilieleza kiwango cha ushiriki kwenye eneo la hatifungani za serikali na binafsi kwa mwaka ulioishia Juni 2023, kiwango hicho kimeongezeka licha ya faida kuwa ya wastani.Jumla ya dhamana za serikali kupitia soko la upili imeongezeka kwa shilingi trilioni 0.1, sawa na ongezeko la asilimia 3.1, hadi shilingi trilioni 3.3 kutoka shilingi trilioni 3.2 mwaka uliopita. Jumla ya thamani za Hatifungani za kampuni binafsi iliongezeka kwa shilingi 0.1, sawa na asilimia 2.5 kutoka shilingi bilioni 0.8 Juni 2022 hadi shilingi bilioni 0.9 mwaka huu. Kuongezeka kwa kiwango cha Hatifungani hizo kulitokana na kuorodheshwa kwa hatifungani mpya za SUKUK na Twiga mwezi Desemba 2022. Hatifungani za kampuni binafsi kwa sasa ni; Jasiri bondi iliorodheshwa na benki ya NMB yenye ukomo wa miaka 3 na kiwango cha faida ya asilimia 8.5 kwa mwaka. Fursa Sukuk bondi iliorodheshwa na banki ya KCB yenye ukomo wa miaka 3 na kiwango cha faida ya asilimia 8.75 kwa mwaka, Twiga bondi iliorodheshwa na benki ya NBC yenye ukomo wa miaka 5 na kiwango cha faida ni asilimia 10 kwa mwaka na bondi ya miaka 5 ya Shirika linalotoa mikopo ya nyumba kwa benki nchini (TMRC) iliorodheshwa kwa awamu kwa asilimia 10.48 na asilimia 11.79.

10.11 Meneja alitoa taarifa kuimarika kwa soko la Hisa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, kulikuwa na kampuni 28 zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) zenye mtaji jumla ya shilingi trilioni 15.0, ukubwa wa mtaji wa soko ulipungua thamani kwa kwa takribani shilingi trilioni 0.6 ikilinganishwa na shilingi trilioni 15.6 zilizorekodiwa mwaka uliopita. Vilevile, katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2023 shughuli za kibiashara katika soko la hisa zilipungua, hii inadhihirishwa na kupungua kwa mauzo kutoka shilingi bilioni 126.6 hadi shilingi bilioni 107.6 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 19.0 (asilimia 15.0). Fahirisi ya Hisa kwa kampuni za ndani za nchi (TSI) ziliongezeka kwa asilimia 4.1 hadi kufikia 4,091.8 huku Fahirisi ya Hisa zote (DSE) ikipungua kwa asilimia 4.0 hadi 1,800.0. Alibanisha kuwa kampuni zilizolipa gawio kwa kipindi cha mwaka mmoja ni TCC (Tsh. 670.0), Twiga ( Tsh.390.0) , TBL(Tsh.290.0), benki ya NMB (Tsh.286.0), SWISS (Tsh. 42.0) na benki ya CRDB (Tsh. 45.0) kwa kila hisa. Hivyo basi, kwa wawekezaji wa aina yote waliowekeza kwenye kampuni tajwa walipata gawio sawa na maelezo hapo juu.

10.12 Taarifa iliendelea kueleza kuwa, hadi kufikia kipindi cha mwaka mmoja ulioshia tarehe 30 Juni 2023, jumla ya rasilimali kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na Taasisi ya UTT AMIS imefikia shilingi bilioni 1,535.4 kutoka shilingi bilioni 996.5. Aidha ,kwa kipindi hicho hicho rasilimali ziliongezeka kwa asilimia 54.0 sawa na shilingi 538.9 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi 383.7 sawa na asilimia 62.6 iliyonakiliwa mwaka uliopita

10.13 Taarifa ya Meneja ilimalizia kwa kuwahakikishia wawekezaji kwenye Mfuko wa Hatifungani kuwa UTTAMIS itaendelea kubuni na kuvumbua fursa stahiki za uwekezaji kadri zinavyojitokeza katika soko ili kuongeza mapato na faida kwa wawekezaji lengo ikiwa ni kuvuka matarajio ya wawekezaji kwa ajili ya maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

## 11.0 MASWALI, MAONI NA MAJIBU

### 11.1 Maswali na Maoni ya Wawekezaji:

11.1.1 Mwekezaji alitaka kujua makubaliano yalioko kwenye mkataba wa makubaliano baina ya UTTAMIS na CRDB ambae ni mwangalizi wa mfuko.

11.1.2 Mwekezaji aliuliza kama gharama za uendeshaji zimechangia kushuka kwa faida kutoka asilimia 14.9 hadi 12.3

11.1.3 Mwekezaji aliomba kufahamu kuhusu mategemeo ya mfuko wa hatifungani kwa mwaka 2024.

11.1.4 Kwenye taarifa ya mapato na matumizi kuna gharama za meneja Shilingi 5,822,733,000/=, Mwekezaji aliomba kupata mchanganuo wa gharama hizo ili iwe rahisi kwa wawekezaji kuweza kushauri namna ya kupunguza gharama kama ikitokea kuna ulazima.

11.1.5 Mwekezaji aliomba kupunguzwa kwa muda wa kufanya repurchase kutoka siku 10 hadi siku 3 kama ilivyo kwenye mfuko wa ukwasi.

11.1.6 Mwekezaji aliomba kupata ufafanuzi kuhusiana na gawio lililo tolewa, maana kwenye ukurasa wa 31 taarifa ya mapato na matumizi, inasema gawio la mapato kwa wenye vipande ni tshs 34,749,875,000/=, lakini ukienda ukurasa wa 34 taarifa ya mtiririko wa mapato, inasema gawio kwa wamiliki wa vipande ni Shilingi 32,943,740,000/=, lakini pia ukurasa wa 36 taarifa ya meneja kuhusu uwekezaji inasema mfuko wa hatifungani umelipa gawio lenye zaidi ya thamani ya Shilingi bilioni 19.1

11.1.7 Mwekezaji aliuliza kama ukosefu wa dola za kimarekani umetupelekea na sisi kuathirika kwenye suala la kushuka kwa faida kutoka asilimia 14.9 hadi 12.3

11.1.8 Mwekezaji aliomba kufahamu kuhusu upatikanaji wa mkaguzi na hua anatumika hadi lini?

11.1.9 Mwekezaji alihoji kuwa kwenye taarifa za fedha upande wa mapato na matumizi, taarifa inaonesha tumepata faida ya bilioni 39.53 na gawio bilioni 34.75 na mapato baada ya kodi tunabaki na bilioni 4.5, kwahiyo mwekezaji alitaka kufahamu hayo mapato baada ya kodi yanaenda wapi?

11.1.10 Mwekezaji aliuliza kwanini wasipewe pesa badala ya chakula katika mikutano?

11.1.11 Mwekezaji aliuliza kuhusiana na utoaji wa elimu ya uwekezaji, aliendelea kuhoji kwamba UTTAMIS ina mpango gani wa kuendelea kutoa elimu kwa vizazi vijavyo?

11.1.12 Mwekezaji alitoa pongezi kwa UTTAMIS kwa uwazi wa taarifa akisema kila kitu kiko wazi kwenye mtandao. Pia alishauri watu watoe pesa kwenye mabenki wazilete UTTAMIS kwasababu kuna faida kubwa, aliongezea akisema tuwe na Imani na taaisisi yetu maana amezunguka mabenki mengi ila UTTAMIS inafaida kubwa zaidi.

11.1.13 Mwekezaji alitoa pongezi kwa mfuko wa hatifungani kwa kutufikia hapa ulipo, maana ni kazi kubwa imefanyika, pia akaongezea akisema kwa wawekezaji ambao ni wafuatiliaji wanaona kazi kubwa UTTAMIS anayoifanya.

11.1.14 Mwekezaji alihoji kwanini aplikesheni ya UTTAMIS hauwezi kuitumia ukiwa nje ya nchi?, akaongezea akisema ni kwasababu inalimit namba za Tanzania peke yake. Aliomba UTTAMIS iwezeshe hiyo aplikesheni iweze kutumika pia na watu waliopo nje ya nchi ili kuweza kumwezesha mwekezaji ambae ni diaspora aweze kufatilia akaunti yake pamoja na kuangalia maendeleo ya uwekezaji wake.

## 11:2 Majibu na Ufafanuzi kwa Maswali na Hoja za wawekezaji

11.2.1 Mwakilishi wa UTTAMIS alianza kwa kufafanua kuwa kwa kawaida katika uanzishaji wa mifuko sheria inataka lazima pawe na mkataba ambao una husisha pande tatu ambapo upande wa kwanza ni meneja wa mfuko ambae atasimamia huo uwekezaji kama UTTAMIS tunavyofanya, upande wa pili ni mwangalizi wa Mfuko ambaye sheria inataka lazima iwe ni Benki na upande wa tatu ni mwekezaji ambae atasoma ule mkataba na kukubaliana na vipengele vilivyomo kabla ya kufanya uwekezaji. Aliendelea kueleza kuwa nyaraka hizi huwa zinatayarisha wakati mfuko unaanza, hivyo kunakuwa na waraka wa makubaliano (trust deed) lakini pia tunakuwa na waraka wa toleo (offer document). Mwakilishi aliendelea kuongeza kuwa hizi nyaraka zipo na wakati tunaanzisha mfuko zinatolewa kwa umma na mara zote tunashauri kila mwekezaji azisome kabla ya kuwekeza. Aliendelea kuelezea kwamba nyaraka hizi zipo kwenye tovuti ya UTTAMIS.

11.2.2 Mwakilishi wa UTTAMIS aliwaeleza wawekezaji kwamba faida za soko lote la fedha kwa mwaka huu wa fedha ambao unaishia June 2023 zimeshuka, akaendelea kusema hali kama hizi huwa zinatokea kulingana na maendeleo ya soko na ni hali ya kawaida kabisa na wala wawekezaji hawana sababu ya kuwa na uwoga. Mwakilishi akaendelea kueleza kua wawekezaji wasiwe na hofu hii faida ya asilimia 12.3 iliyopatikana ni nzuri sana ikilinganishwa na kiwango linganifu na soko. Mwakilishi aliendelea kujibu swali kuhusu gharama za uendeshaji wa mifuko akaeleza kuwa gharama za uendeshaji hazikuchangia kushuka kwa faida ya mfuko. Sheria na kanuni za uendeshaji wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja Tanzania ina mlinda sana mwekezaji na ndio maana unakuta zile gharama zimepewa kikomo yaani kuna mahali gharama zikifika meneja haruhusiwi tena kuongeza gharama kwenye mfuko kwa maana ya kwamba ni lazima azilipe yeye mwenyewe.

11.2.3 Mwakilishi wa UTTAMIS aliwaeleza wawekezaji kuwa kwa sasa mwelekeo ni mzuri na tuna matumani kuwa mwaka ujao yaani 2023/24 hali itakua nzuri zaidi.

11.2.4 Mwakilishi wa UTTAMIS aliwaeleza wawekezaji kwamba taarifa ya hesabu iliyoko kwenye taarifa ya mwaka ya mfuko wa Hatifungani inafupishwa lakini kama Mwekezaji atahitaji taarifa nzima, zinapatikana na zimewekwa kwenye tovuti ya UTTAMIS.

11.2.5 Mwakilishi wa UTTAMIS alieleza kwamba jitihada kubwa za kupunguza muda wa malipo baada ya ununuzi wa vipande yaani repurchase zinafanyika. Mwakilishi aliongeza kuwa maboresho zaidi yatafanyika kadiri mfumo wa kifedha na malipo itavyokuwa na ufanisi zaidi.

11.2.6 Mwakilishi wa UTTAMIS aliwaeleza wawekezaji kwamba taarifa zote zinazoelezea gawio zipo sawa, alianza kueleazea ukurasa wa 31 taarifa ya mapato na matumizi, alisema kuwa hapa tunachukua gharama za gawio zote zilizolipwa na zile ambazo zimetengwa kwajili ya malipo lakini hazijalipwa, katika ukurasa wa 34 taarifa ya mtiririko tunachukua gawio lililolipwa tu, na kwenye taarifa ya meneja ni gawio lililolipwa kwenda kwa wawekezaji.

11.2.7 Mwakilishi wa UTTAMIS aliwaeleza wawekezaji kuwa kukosekana kwa Dola za Marekani hakuna uhusiano na kuathirika kwa faida kwasababu mifuko yote ina wekeza kwa pesa ya Tanzania.

11.2.8 Mwakilishi wa UTTAMIS aliwaeleza wawekezaji kwamba mkaguzi alipatikana kwa kushindanishwa kwenye zabuni na tunaendelea nae maana anafanya kazi nzuri.

11.2.9 Mwakilishi wa UTTAMIS aliwaeleza wawekezaji kwamba mapato yanapopatikana, gharama zote zinatolewa halafu faida wanapewa wawekezaji, akaendelea kwa kusema mfano kwa mwezi faida ya asilimia 1.02 ikipatikana, hapo asilimia 1 tunatoa kama gawio kwa wawekezaji halafu asilimia 0.02 inabaki kwenye mtaji wako. Kwahiyo, bilioni 4.5 ndiyo ilikuwa ongezeko la mtaji na imebaki kwenye mtaji wako.

11.2.10 Mwakilishi wa UTTAMIS aliwaeleza wawekezaji kwamba taratibu na miongozo ya uendeshaji wa mifuko hairuhusu utoaji wa fedha badala ya chakula katika mikutano.

11.2.11 Mwakilishi wa UTTAMIS alieleza kua elimu ya uwekezaji kwa ujumla kwa Tanzania haina muda mrefu sana, lakini jitihada kubwa zimeelekezwa katika utoaji wa elimu ya fedha na uwekezaji kwa wananchi na vijana vyuoni.

11.2.12 Mwakilishi wa UTTAMIS alipokea pongezi kutoka kwa mwekezaji juu ya uwazi wa taarifa tunazotoa kwa wawekezaji wetu na umma kwa ujumla.

11.2.13 Mwakilishi wa UTTAMIS alipokea pongezi kutoka kwa mwekezaji na kuongeza kuwa jitihada zitaendelea kufanyika ili kupata faida nzuri zaidi.

11.2.14 Mwakilishi wa UTTAMIS alipokea maoni kuhusu aplikesheni ya UTTAMIS kuweza kutumika nje ya nchi kwa diaspora na kuhaidi kuyafanyia kazi kwa kuwawezesha diaspora kufatilia uwekezaji wao na kufanya uwekezaji katika mifuko ya UTTAMIS bila kupata changamoto yoyote.

## 12.0 KUFUNGA MKUTANO

Kwa kuwa hakukuwa na masuala zaidi ya kujadili, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwashukuru Wawekezaji wote kwa kuhudhuria katika Mkutano huo. Pia aliwahakikishia ya kuwa mawazo na mapendekezo yaliyotolewa katika Mkutano yatazingatiwa na yale yanayowezekana yatatekelezwa. Mwisho aliwatakia heri ya sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya 2024. Mkutano ulifungwa saa 11:37 jioni.

| ................................. | ................................. |
|---|---|
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

.................................

**TAREHE**

## KIAMBATISHO “A”

# ORODHA YA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA HATIFUNGANI WALIOHUDHURIA KWENYE MKUTANO WA NNE (4) WA MWAKA WA MFUKO ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MWALIMU NYERERE, DAR ES SALAAM TAREHE 18 NOVEMBA 2023

| S/NO | JINA LA MWEKEZAJI |
|---|---|
| 1 | ABDALLAH DAVID MLANGWA |
| 2 | ABDALLAH MOHAMED ALPHONCE |
| 3 | ABDUL SAID MUSHI |
| 4 | ABDULKADIR SULEIMAN MBEO |
| 5 | ABDULRASHID HAMZA RASHID |
| 6 | ABEDINEGO FABIAN AHIA |
| 7 | ABEL EMMANUEL MWAKIFWAMBA |
| 8 | ABELA JASSON BOCKO |
| 9 | ABRAHAM ALEX MWANYIKA |
| 10 | ABUBAKAR JABU NYUNDO |
| 11 | ABUBAKAR MUSSA MAGHUMBI |
| 12 | ADAM WILFRED KISWAGA |
| 13 | ADELAIDA EVARISTI MASAWE |
| 14 | ADELAIDA JOYCE KAGARUKI |
| 15 | ADRIEL RONALD FUGARA |
| 16 | ADROPHINA SALVATORY KYEBIROHI |
| 17 | AGABITI VICENT PAUL |
| 18 | AGATHA CLAUD SWAI |
| 19 | AGATHA PETER MTINDI |
| 20 | AGNES ALEX KALINGA |
| 21 | AGNES BERNAD MASAWE |
| 22 | AGNES KONDOWE PONERA |
| 23 | AGNES LAWRANCE CHIBWANA |
| 24 | AGNES MICHAEL MPAZI |
| 25 | AGNES WENCESLAUS MAYO |
| 26 | AGNESS HILARY KOLOMBANI |
| 27 | AGNESS KOKUHILWA REMIGIUS |
| 28 | AGNESS MKATULIA SHIO |
| 29 | AGRICOLA AFRICANUS MUSHI |
| 30 | AGRICOLLA EMILIAN ASSENGA |
| 31 | AHADI RAMADHANI KATIGIRI |
| 32 | AHMAD JUMA MCHALAGANYA |
| 33 | AHMADI YUSUFU MTOTA |
| 34 | AHMED HASSANI ABEID |
| 35 | ALBENTINA LEONARD MWAKIBETE |
| 36 | ALBERT ANACLET IKONJE |
| 37 | ALBERT ANACLET IKONJE (Rep. Subira Joseph) |
| 38 | ALBERT HASSAN MILANZI |
| 39 | ALBERT OSWARD MAKWAYA |
| 40 | ALBERTA NDESARIO KINABO |
| 41 | ALEX BEATUS WAMBOY |
| 42 | ALEX NDYETABULA NGAIZA |
| 43 | ALFEO JUMA MUSSA |
| 44 | ALFRED TIMOTHY CHUNGA |
| 45 | ALLAN LUKA MWAIGAGA |
| 46 | ALLAN RODERICK MAMUYA |
| 47 | ALLEN COLMAN SWAI |
| 48 | ALLIANCE INSURANCECORPORATION LIMITED |
| 49 | ALLY HASSAN NAMANGAYA |
| 50 | ALLY MOHAMED MAPE |
| 51 | ALLY RAJABU MSUYA |
| 52 | ALLY RASHID MAMU |
| 53 | ALODIA JUSTUS WAMARA |
| 54 | ALOYS STANISLAUS BUPAMBA |
| 55 | ALPHA MPONZA AGUSTINO |
| 56 | ALPHAXARD AMOS MWITA |
| 57 | ALPHONCE ALEXANDER ASSENGA |
| 58 | ALPHONCE IGNAS MUSIBA |
| 59 | ALPHONCE JOSEPH MABULA |
| 60 | ALPHONCE TEOBARD MWAGENI |
| 61 | AMANI ANAELI MLAKI |
| 62 | AMANI ELIMELECK NJABILI |
| 63 | AMANI ISAYA MKOLA |
| 64 | AMANI MATUTU MAHUNDA |
| 65 | AMIDA HENERIKO KAGUNDA |
| 66 | AMINA HATIBU OTHUMANI |
| 67 | AMINA JUMA MSANGI |
| 68 | AMINA KUTETA KYARUZI |
| 69 | AMORI EDWARD MALEYEKI |
| 70 | Amos Paul Nyanda |
| 71 | ANAEL PHILEMON MEENA |
| 72 | ANANDE DANIELI MBISE |
| 73 | ANASTAS JOHNSON XIBONA |
| 74 | ANDREAS JOHN HAULE |
| 75 | ANDREW ANTHONY MALAMLA |
| 76 | ANDREW SILVANO MTALI |
| 77 | ANDY ACKIM MWANDEMBWA |
| 78 | ANESI SATOKI MAHENGE |
| 79 | ANETH MZUMA LWITAKUBI |

| | |
|---|---|
| 80 | ANGELA PHILIPO MWAIKAMBO |
| 81 | ANGELINA HOLLO KIVANDA |
| 82 | Angelina Julius Qambade |
| 83 | ANGELINA ROGERS SHEHUMU |
| 84 | ANIFA SELEMANI MKINGA |
| 85 | ANNA ALEX HAULE |
| 86 | ANNA BALTAZARY MASSAWE |
| 87 | ANNA CHARLES KINYAHA |
| 88 | ANNA IBRAHIM SILAYO (Rep. Rehema Silayo) |
| 89 | ANNA JONASAI MAPHOLE |
| 90 | ANNA LAWRENCE MUHOJA |
| 91 | Anna M Mrema |
| 92 | ANNA MAJWALA CASSIAN |
| 93 | ANNA MBEDE KIKWA |
| 94 | ANNA MESHACK KAGYA |
| 95 | ANNA NAFTAL KAWICHE |
| 96 | ANNA PANTALEO MATERU |
| 97 | ANNA RAJABU MBURA |
| 98 | ANNA RAMADHANI ZAIPUNA |
| 99 | ANNAMOLISIA KENAN CHENGULA |
| 100 | ANNASTAZIA ANGETELILE KAJANGE |
| 101 | ANNE BENEDICT MUTALEMWA |
| 102 | ANNE HERBERT MAPUNDA |
| 103 | ANNE YOLAMU SWILLA |
| 104 | ANNES ANDREA MWALONGO |
| 105 | ANNETH MASALU MALIMI |
| 106 | ANSELMI GABRIEL LAIZER |
| 107 | ANSHIMINKYA ANDERSON KIMARO |
| 108 | ANTHONY MASERO MABOTO |
| 109 | ANTHONY PETER SIYOVELWA |
| 110 | ANTHONY YUDATADE NDESINGO |
| 111 | APANSIA JONATHAN NDOSSA |
| 112 | APASIA IGNATIO KAGONJI |
| 113 | APOLINARY KLARENSI TAMAYAMALI |
| 114 | AQUILINA IGNAS OTTARU |
| 115 | ARBOGAST ZACHARIA MSANGAWALE |
| 116 | ARON MOSES NASSARY |
| 117 | ASHA KHALFANI MZIRAY |
| 118 | ASHA RAMADHANI CHOMOLA |
| 119 | ASIA JUMA IDDI |
| 120 | ASWILE EZEKIA MWAMBEMBE |
| 121 | ATHANAS EVARIST BAGENYI |
| 122 | ATHANASIA PETER NGOWI |
| 123 | ATHUMAN MAULID SHABAN |
| 124 | ATU SIMON MWAIPYANA |
| 125 | AUDA PONELA KILAGWA |
| 126 | AUDIPHACE CLAUDI MUSHI |

| | |
|---|---|
| 127 | AUGUST BENEDICT KOWERO |
| 128 | AURELIA HIPOLITE MUSHI |
| 129 | AYOUB ISSA MDEMU |
| 130 | AZIZA OMARI NGONYANI |
| 131 | BADRIANA SYLVESTER KAIMUKILWA |
| 132 | BAKARI OTHMANI HASSANI |
| 133 | BAKARI SALIMU MOKIWA |
| 134 | BARAKA MARCO MALANYINGI |
| 135 | BARAKA RAJAB BARAKA |
| 136 | BEATHER SENGEREMA KISHUSHU |
| 137 | BEATRICE MASHISA KASHINJE |
| 138 | BELANDO MICHAEL NARDO |
| 139 | BENEDICTO PASTORY MWESIGA |
| 140 | BENEDICTO RENATUS RAPHAEL |
| 141 | BENEDICTO SONZWE MAHELA |
| 142 | BENSON LUGOBI NALLYA |
| 143 | BERNADETH SEBASTIAN MATTO |
| 144 | BERNARD PIUSI MSIGWA |
| 145 | BERTHA FREDERICK MAMUYA |
| 146 | BERTHA THERESA KASAMBALA |
| 147 | BERTIN ALFRED MUSHI |
| 148 | BESTUS RWENYAGILA KALOKOLA |
| 149 | BETRAM BONAVENTURA KISWAGA |
| 150 | BETTY REGINALD MCHAKI |
| 151 | BINDO SELEMANI MAMBOLEO |
| 152 | BLANDINA BERNARD ZACHARIA |
| 153 | BONAVENTURA BENEDICT ISHENGOMA |
| 154 | BONAVENTURA PHILIP SAGAMILWA |
| 155 | BONAVENTURE ISDORY MSIGWA |
| 156 | BONIFACE ELISARIA MREMA |
| 157 | BONIFACE MATTLE YUMBA |
| 158 | BRENDA JOHN SASI |
| 159 | BRIAN DAMAS BENJAMIN |
| 160 | BRIAN KULWA MOSHI |
| 161 | BRIGHTSUCCESS GABRIEL EDWARD |
| 162 | BRIGITA NICHOLAUS MAKYAO |
| 163 | BRIGITHA STEVEN MREMA |
| 164 | BRUNO THADEUS MMASSY |
| 165 | Bruno Yusuph Mchatta |
| 166 | BRYAN CHRISTIANUS NTWENYA |
| 167 | BUGUMBA JUMANNE MASHAMBA |
| 168 | BUMA INVESTMENT COMPANY LIMITED |
| 169 | BYERA RAHEL MUGINI (Rep. Allan Mhilu) |
| 170 | CALISTA LUDOVICK MAKUNDI |
| 171 | CAREN MELKIZEDECK MARANDU |
| 172 | CAROLYNE ANATHE GAMBA |
| 173 | CAROLYNE CHARLES SINGH |

| | |
|---|---|
| 174 | CAROLYNE NAIMAN MKIRAMWENI |
| 175 | CATHERINE JOSEPH NANGALI |
| 176 | CATHERINE MARCO VINGILLAH |
| 177 | CATHERINE MOHAMED RUTENGE |
| 178 | CATHERINE MOSHIRO MBUNDA |
| 179 | CATHERINE PATRICK MWAIPOPO |
| 180 | CATION AND TRANSPORT WORKER'S UNION OF Z |
| 181 | CECILIA KEMILEMBE RUGEMALIRA |
| 182 | CECILIA NAKANWAGI KIIZA |
| 183 | CECILIA ROMAN AKARO |
| 184 | CECILIA YONA MWENISONGOLE |
| 185 | CHARLES MARTIN GENGE |
| 186 | CHARLES MAYENGA NGASSA |
| 187 | CHARLES YOHANA MHINA |
| 188 | CHARLES YOHANA PASCHAL |
| 189 | CHEGERO ALPHONCE MKAMA |
| 190 | CHEKA MWAMBUNGU CHAGGE |
| 191 | CHRISTINA DAUD KIMARO |
| 192 | CHRISTINA JULIUS OTACHO |
| 193 | CHRISTINA NGHELEMBI JOSEPH |
| 194 | CHRISTINE NANYIKA HAMZA |
| 195 | Christopher Dunny Mmbaga |
| 196 | CHRISTOPHER JOHN MWAMBAPA |
| 197 | CHRISTOPHER LAWRANCE KANNONYELE |
| 198 | CHRISTOPHER MWITA MOSORE |
| 199 | CLARICEEVETHA KENAN CHENGULA |
| 200 | CLEMENCE QUADRATES KAHAMA |
| 201 | CLEMENT ASUKENYE KIBONA |
| 202 | CLEMENT GERHARD MPUNGA |
| 203 | CLEMENT LAWRENCE KAMULI |
| 204 | CLEOPHAS KAMUHABWA NSHEKA |
| 205 | CLIFF AHMED CHILIPACHI |
| 206 | COFFEE AND WINE CLUB |
| 207 | COLETA ROMAN MOMBURI |
| 208 | COLETHA EVARIST MISSANA |
| 209 | COLETHA JEREMIAH CHUMA |
| 210 | Colman Mrana Ngainayo |
| 211 | CONSOLATA CHRISTINA JOSEPH |
| 212 | CONSOLATA ELIAS MBENA |
| 213 | Cosmas Silvestar Komba |
| 214 | COSTA NEHEMIA MUNISI |
| 215 | CRDB INSURANCE COMPANY LIMITED |
| 216 | CRISPIN BRUNO MOMBE |
| 217 | DAFROSA CONRAD MANENO |
| 218 | DAKULU PHILIP MBELWA |
| 219 | DALILA HUSSEIN MIRRY |

| | |
|---|---|
| 220 | DALISO JOYCE MWIDADI |
| 221 | DAMAS JUMA KAYERA |
| 222 | Daniel Eliabu Urio |
| 223 | DANIEL GODFREY MANDARI |
| 224 | DANIEL JOSEPH MUGANYIZI |
| 225 | DANIEL RICHARD JUMA |
| 226 | DANIEL SAMWEL ZAKARIA |
| 227 | DARIO BATHROMEO MWANJELILE |
| 228 | DASTO CHAULA MWAKABANA |
| 229 | DAUDI FRANKLIN MTEI |
| 230 | DAUDI MUTALEMWA RWIZA |
| 231 | DAUDI NGWANDU SAGUDA |
| 232 | DAUDI YAKOBO NDAGAMBANIWE |
| 233 | DAVID GREYSON MNZAVA |
| 234 | DAYANA JACTAN KIHOMBO |
| 235 | DCTW SACCOS LTD |
| 236 | DEMETRIA KOKULAMUKA NGILWA |
| 237 | DENICE CYPRIAN KAMUGUMYA |
| 238 | DEODATUS KENAN CHENGULA |
| 239 | DEOGRATIAS RUTA WILLIAM |
| **Jumla ya Mapato** | **84,046,581** | **48,351,089** |
| | | |
| Gharama za Meneja | (9,836,645) | (5,822,733) |
| Gharama za Mwangalizi wa Mfuko | (546,480) | (323,485) |
| Gharama za Mauzo ya Dhamana na Hisa | (309,308) | (112,467) |
| Gharama za Ukaguzi wa Hesabu | (61,523) | (52,497) |
| Gharama za Mauzo ya Vipande | (3,833,649) | (1,938,642) |
| Gharama nyinginezo za Uendeshaji | (942,307) | (573,707) |
| **Jumla ya Gharama za Uendeshaji** | **(15,529,912)** | **(8,823,531)** |
| | | |
| **Mapato halisi kabla ya gawio kwa wenye Vipande** | **68,516,669** | **39,527,558** |
| Gawio la mapato kwa wenye vipande | (57,243,416) | (34,749,875) |
| **Mapato halisi kabla ya Kodi** | **11,273,253** | **4,777,683** |
| | | |
| Kodi ya Zuio | (277,322) | (243,403) |
| **Mapato halisi baada ya Kodi** | **10,995,931** | **4,534,280** |
| | | |
| Mapato mengineyo (other comprehensive income) | - | - |
| **Ongezeko halisi la thamani ya Mfuko** | **10,995,931** | **4,534,280** |

# URARI WA HESABU ZA MFUKO (BALANCE SHEET)
# MNAMO TAREHE 30 JUNI 2024

| | 2024<br>TSH '000 | 2023<br>TSH '000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali za Mfuko** | | |
| Fedha Taslim | 75,278,457 | 1,942,848 |
| Dhamana za Serikali | 595,871,541 | 417,819,814 |
| Amana kwenye Mabenki za Muda Maalum | 5,000,000 | 8,000,000 |
| Rasilimali Nyinginezo (Other Receivable) | 303,768 | 1,862,489 |
| **Jumla ya Rasilimali** | **676,453,766** | **429,625,151** |
| | | |
| **Dhima ya Mfuko** | | |
| Dhima | (10,025,951) | (8,869,050) |
| **Jumla ya Dhima ya Mfuko** | **(10,025,951)** | **(8,869,050)** |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **666,427,815** | **420,756,101** |
| | | |
| **Inawakilishwa na:** | | |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **666,427,815** | **420,756,101** |
| **Idadi ya Vipande** | **5,685,741,558** | **3,662,034,187** |
| **Thamani ya Kipande** | **117.21** | **114.90** |

# TAARIFA YA MABADILIKO YA THAMANI YA MFUKO (STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSETS ATTRIBUTABLE TO UNIT HOLDERS) KWA MWAKA ULIOSHIA 30 JUNI 2024

| | 2024<br>TSH '000 | 2023<br>TSH '000 |
|---|---|---|
| **Thamani ya mfuko Julai 1** | **420,756,101** | **218,690,997** |
| Marekebisho ya Mwaka uliopita | 10,995,931 | 4,534,280 |
| Mabadiliko/Ongezeko ya thamani ya mfuko | 431,752,032 | 223,225,277 |
| | | |
| **Miamala (Transactions) ya wenye vipande kwa mwaka** | | |
| Mauzo ya vipande (Sales) | 405,804,664 | 248,172,474 |
| Ununuzi ya vipande (Repurchase) | (171,128,881) | (50,641,650) |
| **Mabadiliko ya thamani ya mfuko** | **234,675,783** | **197,530,824** |
| **Thamani halisi ya Mfuko** | **666,427,815** | **420,756,101** |

# TAARIFA YA MTIRIRIKO WA MAPATO (CASH FLOW STATEMENT) KWA MWAKA UNAOISHIA 30 JUNI 2024

| | 2024<br>TSH '000 | 2023<br>TSH '000 |
|---|---|---|
| **FEDHA ITOKANAYO NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | |
| Mapato baada ya Kodi | 10,995,931 | 4,534,280 |
| **Imerekebishwa na:** | | |
| Gawio kwa Wawekezaji | 57,243,416 | 34,749,875 |
| Gharama za Kodi ya Zuio | 277,322 | 243,403 |
| Mapato yatokanayo na riba (effective interest rate method) | (68,788,113) | (40,328,908) |
| **Faida kabla ya mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji:** | **(271,444)** | **(801,350)** |
| **Mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji** | | |
| Ongezeko kwa Dhamana za Serikali | (175,308,936) | (230,584,433) |
| Amana za Muda Maalumu kwenye Mabenki | 3,000,000 | 17,000,000 |
| Ongezeko kwa dhima ambazo mfuko haujalipa | 1,558,721 | 3,823,082 |
| Ongezeko la Rasilimali nyinginezo | (859,298) | (1,824,047) |
| **Fedha iliyotumika kwenye shughuli za uendeshaji** | **(171,880,957)** | **(212,386,748)** |
| Kodi iliyolipwa hadi sasa | (277,322) | (243,403) |
| Mapato yaliyopokelewa kutokana na riba | 66,045,322 | 47,676,470 |
| **Fedha halisi iliyotumika katika shughuli za uendeshaji** | **(106,112,957)** | **(164,953,681)** |
| **AMANA YA MFUKO (FINANCING ACTIVITIES)** | | |
| Mauzo ya Vipande (Sales of Units) | 405,804,664 | 248,172,474 |
| Ununuzi (Repurchase) wa Vipande | (171,128,881) | (50,641,650) |
| Gawio kwa wamiliki wa vipande | (55,227,217) | (33,041,326) |
| **Fedha/Amana halisi toka kwa wenye vipande** | **179,448,566** | **164,489,498** |
| **Ongezeko halisi la Fedha** | **73,355,609** | **(464,183)** |
| **Salio la fedha mwanzoni mwa Mwaka** | **1,942,848** | **2,407,031** |
| **Salio la fedha mwishoni mwa Mwaka** | **75,278,457** | **1,942,848** |

.....................................
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** 8 Novemba, 2024

.....................................
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** 8 Novemba, 2024

# 8 Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji

FUND
More ideas for your money

# Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji


Mfuko wa Hatifungani ni mfuko wa wazi unaojikita zaidi kuwekeza kwenye dhamana za serikali za muda mrefu, hatifungani za kampuni binafsi na kiasi kwenye soko la fedha. Mfuko ulianzishwa Septemba 2019 na hutoa fursa kwa wawekezaji kukuza mtaji pamoja na kupata gawio. Mwekezaji huchagua mojawapo kati ya aina tatu za mpango (a) Gawio la kila mwezi (b) Gawio la kila nusu mwaka (c) Kukuza mtaji.

Mahitaji ya awali ya uwekezaji ni shilingi elfu hamsini (50,000/=) na kiwango cha nyongeza kisichopungua shilingi elfu tano (5,000/=) kwa wawekezaji wenye mpango wa kukuza mtaji tu. Mwekezaji anaruhusiwa kuchukua fedha zake wakati wowote anaohitaji na bila kutozwa gharama za kutolea [exit load], hivyo kudhihirisha kuwa mfuko wa Hatifungani ni fursa maridhawa kwa wawekezaji.

## 1.0 Ukubwa wa mfuko na Thamani ya Kipande

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, mfuko wa Hatifungani ulikuwa na ukubwa wa shilingi bilioni 670.3. Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2024 ukubwa wa Mfuko umeongezeka kwa shilingi bilioni 246.7 sawa na asilimia 58.2 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 203.8 mwaka 2023. Kwa mwaka 2024, thamani ya kipande imeongezeka kwa 14.3 hadi kufikia shilingi 118.1 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi 14.0 mwaka 2023. Aidha, kwa muda huo Mfuko umelipa gawio la shilingi 12 kwa kila kipande.


*Chati Na. I: Ukuaji wa Mfuko wa Hatifungani tangu kuanzishwa hadi Juni, 2024*




## 2.0 Mgawanyo wa Uwekezaji

Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 mwezi Juni 2024, UTT AMIS kama meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi katika kufikia mgawanyo anuai wa rasilimali kwa matakwa ya sera za mfuko wa Hatifungani. Mgawanyo anuai wa rasilimali za Mfuko mwezi Juni 2024 ulikuwa kama inavyoonekana kwenye chati namba II hapo chini:-

*Chati Na. II: Mgawanyo wa Uwekezaji wa mfuko wa Hatifungani hadi tarehe 30 Juni 2024*



Chati namba II, inaonesha mgawanyo wa uwekezaji katika mfuko wa Hatifungani ambapo asilimia 89.5 imewekezwa katika dhamana za serikali za muda mrefu, ikifuatiwa na asilimia 9.7 kwenye amana za benki za muda mfupi na asilimia 0.8 kwenye amana za benki za muda maalumu. Aidha, chati hiyo inaonesha kiwango kikubwa cha asilimia kimewekezwa kwenye dhamana za serikali za muda mrefu ili kuimarisha kiwango cha faida na mapato ya mfuko.

**KUANZISHWA;**

**SEPTEMBA 2019**

**30 JUNI 2024**

**BEI YA KIPANDE**

**SHILINGI 118.1**

**UKUBWA WA MFUKO SHILINGI BILIONI 670.3**

**GAWIO**

**KWA MWAKA SHILINGI BILIONI 28.2**

**FAIDA KWA**

**MWAKA**

**12.5%**

## 3.0 Faida

Kiwango cha faida kwa kipindi cha mwaka mmoja ni asilimia 12.5 ikilinganishwa na faida ya asilimia 12.3 mwaka 2023. Aidha, kiwango cha faida kwa mwaka 2024 cha asilimia 12.5 ni zaidi ya kigezo cha ufanisi cha asilimia 12.3 kama inavyonekana kwenye jedwali namba I.

Jedwali namba I na II, linaonesha mwenendo wa utendaji wa Mfuko, kigezo cha ufanisi (benchmark) na maeneo mengine linganifu kwa mwaka 2020 hadi 2024. Hali ya utendaji wa Mfuko inaonekana ni nzuri na shindani ikilinganishwa na faida ya kigezo cha ufanisi na maeneo linganifu sokoni.

***Jedwali Na. I: Faida za Mfuko wa Hatifungani kwa kipindi tangu Juni, 2021 hadi Juni, 2024***

| Na | Mwaka wa Fedha | Ukubwa wa mfuko Shilingi Bilioni | Hali ya Utendaji | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Faida | Kigezo cha ufanisi |
| 01. | 2023/24 | 670.3 | 12.5% | 12.3% |
| 02. | 2022/23 | 423.6 | 12.3% | 9.7% |
| 03. | 2021/22 | 219.8 | 14.9% | 9.3% |
| 04. | 2020/21 | 94.5 | 15.7% | 10.1% |

*Kumb:kigezo cha ufanisi ni faida kwenye dhamana ya serikali ya miaka 10.*

Ili kupima mafanikio ya Mfuko inabidi kulinganisha na viwango vya faida vinavyotolewa na soko kwenye amana za benki na dhamana za serikali kama vinavyoonekana kwenye Jedwali namba II hapo chini:

***Jedwali Na. II: Viwango vya faida katika dhamana za Serikali na amana za benki***

| Maelezo | Kwa Mwaka Wa Fedha Ulioisha Mwezi Juni | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 10 | 11.5% | 10.3% | 11.1% | 12.3% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 7 | 10.1% | 9.3% | 9.7% | 9.7% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 5 | 9.2% | 8.9% | 9.7% | 10.0% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 2 | 7.9% | 4.4% | 9.1% | 11.6% |
| Dhamana ya Serikali ya Mwaka 1 | 4.8% | 4.7% | 6.9% | 8.3% |
| Amana za benki | 2.2% | 1.5% | 1.6% | 2.8% |

*Chanzo; Benki Kuu ya Tanzania*

Mambo mengine muhimu ya kuzingatia wakati wa kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Hatifungani na faida zitokanazo na uwekezaji kwenye amana katika benki;

- Viwango vya faida vilivyoonyeshwa hapo juu ni kabla ya kutoa kodi ya zuio (withholding tax) ya asilimia 10.0 wakati mapato ya mfuko wa Hatifungani ni baada ya kutoa kodi ya zuio ya asilimia 10.0
- Mfuko wa Hatifungani unaruhusu wawekezaji wake kuuza vipande vyao wakati wowote hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata fedha pindi anapozihitaji.
- Hakuna gharama wakati wa kuingia na kutoka katika mfuko.
- Aina nyingine za uwekezaji katika soko ya fedha zina muda maalumu na ukomo, uwekezaji katika mfuko wa Hatifungani hauna muda maalumu wala ukomo.
- Urahisi wa kuongeza na kutoa fedha, aidha mtu anaweza kununua na kuuza vipande.
- Faida kwenye Mfuko utolewa sawa kwa wawekezaji wote (wenye mtaji na kipato kidogo, wa kati na hata wale wenye mtaji na kipato kikubwa).

## 4.0 Mwenendo wa Uchumi, Tanzania

### 4.1 Pato la Taifa

Kwa mwaka 2023 uchumi ulikua kwa asilimia 5.1, ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2022. Aidha, sababu zilizochagia ukuaji huo ni pamoja na kuwepo kwa hali nzuri kwenye shughuli za madini, kilimo na ujenzi. Mambo mengine yaliyosababisha ukuaji wa uchumi ni kuwepo kwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwenye miundombinu na shughuli zingine za kijamii nchini.

Hata hivyo, ukuaji wa uchumi mwaka 2023 unaonesha kuwa nchi imetekeleza sera madhubuti na imehimili madhara yatokanayo na vita zinazoendelea ulimwenguni. Hivyo, kwa mwaka 2024 kiwango cha ukuaji wa uchumi kinakadiriwa kukua kwa asilimia 5.4.

Hali hii ya mwenendo wa uchumi ni muhimu kwa mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS kwani inaonesha matarajio mazuri ya faida kwa wawekezaji.

***Jedwali Na. III: Mwenendo wa Uchumi, Tanzania***

| Mwaka | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pato halisi la Taifa | 7.0% | 7.0% | 4.8% | 4.9% | 4.7% | 5.1% | *5.4% |

*Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki kuu ya Tanzania*

### 4.2 Mfumuko wa Bei

Jedwali na. IV hapo chini linaonesha hali ya mfumuko wa bei kwa kipindi tangu mwaka 2018 hadi 2024, kwani mfumuko wa bei nchini umebaki chini ya asilimia 5.0. Aidha, kiwango hicho ni stahimilivu na kipo chini ya asilimia 5.0 ya kigezo linganifu kinachotumika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya maendeleo kusini mwa Afrika (SADC).

Mwenendo huu wa mfumuko wa bei umetokana na kuwepo kwa hali nzuri kwenye shughuli za kilimo na sera madhubuti. Aidha, mamlaka inakadiria hali ya mfumuko wa bei kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano ijayo kubaki chini ya asilimia 5.0. Kuwepo kwa hali nzuri ya mwenendo wa mfumuko wa bei nchini kumewezesha wawekezaji kuendelea kuwekeza kwa wingi. Hata hivyo.

***Jedwali Na. IV: Hali ya Mfumuko wa Bei***

| Mwaka | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa Bei | 3.7% | 3.7% | 3.2% | 3.6% | 4.4% | 3.6% | 3.1% |

*Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

### 4.3 Sekta ya benki

Katika mwaka wa fedha ulioisha Juni 2024, sekta ya benki ambayo inajumuisha sehemu kubwa zaidi ya sekta ya huduma ya fedha ilibaki imara, thabiti na yenye faida, ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha. Jumla ya rasilimali ziliongezeka kwa shilingi trilioni 8.3 kutoka shilingi trilioni 53.7 iliyonakiliwa Juni 2023 hadi shilingi trilioni 62.0 Juni 2024. Kiasi cha amana za wateja kiliongezeka kwa asilimia 13.7 kutoka shilingi trilioni 35.7 hadi shilingi trilioni 40.6 Juni 2024. Mikopo kwa wateja ilifikia shilingi trilioni 37.4 ikilinganishwa na shilingi trilioni 31.5 mwaka uliopita. Mifumo ya malipo kwa njia ya kidigitali nchini iliendelea kuwa imara, ikithibitishwa na kuwepo kwa kiwango cha juu cha miamala iliyokamilika kwa muda mfupi. Kuwepo kwa mifumo imara na thabiti kumehamasisha umma kuendelea kuamini na kutumia mifumo ya kidigitali kwenye huduma mbalimbali za kifedha. Aidha, mwaka 2023 idadi ya miamala iliyofanyika kutoka kwenye huduma za pesa mtandao kwenda benki ni milioni 6.6 yenye thamani ya shilingi trilioni 2.7. Kwa kipindi hicho, idadi ya miamala iliongezeka kwa asilimia 34.1 na asilimia 25.2 kwenye thamani.

Kuendelea kuimarika kwa sekta ya benki nchini ni muhimu kwa mifuko na wawekezaji kwa ujumla, kwani hali hio husaidia kuchochea shughuli za uchumi na huwarahisishia kuwekeza kwenye mifuko ya UTT AMIS kwa urahisi.

Meneja wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja amefanikiwa kuunganisha mifumo ya UTT AMIS na benki ili kuwawezesha wawekezaji kununua vipande kwa njia ya kidigitali popote walipo.

### 4.4 Sekta ya Mawasiliano

Katika sekta ya mawasiliano, idadi ya laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa imeongezeka kwa milioni 11.5 hadi kufikia milioni 75.5 mnamo Juni 2024 ikilinganishwa na ongezeko la laini milioni 7.8 mwaka uliopita. Aidha, idadi ya laini hizo za simu zilizosajiliwa ni zile zilizotumika angalau mara moja katika miezi mitatu iliyopita. Usajili wa akaunti za huduma za pesa mtandao (idadi ya akaunti) umeongezeka kwa asilimia 18.0 kutoka milioni 47.2 hadi milioni 55.7 mnamo Juni 2024.

Jumla ya mauzo ya vipande yaliyopokelewa na UTT AMIS kupitia mitandao ya simu za mkononi ni shilingi bilioni 47.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25.4 yaliyopokelewa mwaka 2023.

Kwa kipindi chote, ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini umeleta matokeo chanya kwa Taasisi ya UTT AMIS kwani imechochea na kurahisisha uwekezaji katika mifuko na kuboresha zaidi huduma binafsi. Kupitia simu za mkononi wawekezaji wanaweza kufungua akaunti, kuuza vipande, kuangalia salio na miamala waliofanya kwa kupiga *150*82# au kutumia programu tumizi (UTT AMIS APP) pamoja na kununua vipande kupitia huduma ya pesa mtandao. Pia, UTT AMIS inatarajia kuongeza kiwango cha kutoa fedha kwenye uwekezaji (kuuza vipande) kwa siku kutoka kiwango kinachotumika sasa cha shilingi milioni 2 hadi milioni 5 kupitia simu za mkononi.

### 4.5 Dhamana za Serikali

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioisha Juni 2024, uwekezaji kwenye dhamana za serikali katika soko la awali ulifanyika kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Kiasi cha dhamana za serikali za muda mfupi kilichouzwa kilipungua kwa shilingi trilioni 0.6 hadi shilingi trilioni 2.7. Hata hivyo, uhitaji wa dhamana za serikali za muda mfupi uliongezeka kwa shilingi trilioni 0.7 hadi kufikia shilingi trilioni 4.3 kutoka shilingi trilioni 3.6 mwaka jana. Kiasi kilichokubaliwa baada ya mnada kimeongezeka kwa shilingi trilioni 0.1 kutoka shilingi trilioni 2.5 hadi shilingi trilioni 2.6 Juni 2024.

Katika soko la dhamana za serikali za muda mrefu, jumla ya shilingi trilioni 3.3 ziliuzwa ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.3 mwaka uliopita. Kiasi cha ushiriki kwa kipindi hicho kiliongezeka kwa shilingi trilioni 0.6 hadi shilingi trilioni 5.2 ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.6 mwaka uliotangulia. Kiwango kilichokubaliwa kilipungua kwa shilingi trilioni 1.1 hadi shilingi trilioni 2.8 kutoka shilingi trilioni 3.9 mwaka 2023.

Kuongezeka kwa ushiriki na uwekezaji kwenye dhamana za serikali kunaashiria ongezeko la uelewa kwa umma kuhusu uwekezaji na akiba. Hivyo, ongezeko la uelewa na ushiriki katika soko la dhamana nchini husaidia kuboresha ukwasi na faida kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

More ideas for your money

### 4.6 Viwango vya Riba na Faida

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioisha Juni 2024, viwango vya riba vinavyotozwa kwenye mikopo na faida zinazotolewa kwenye amana za benki hazikubadilika kwa kiwango kikubwa.

Wastani wa riba za mikopo ulikuwa asilimia 15.4 na riba kwa mkopo wa mwaka mmoja ni asilimia 15.8. Wastani wa faida kwa amana za benki ni asilimia 7.5 na faida kwa amana ya mwaka mmoja ni asilimia 8.7.

Kiwango cha wastani wa faida kwenye dhamana za serikali za muda mfupi kiliongezeka hadi asilimia 8.3 mnamo Juni 2024 kutoka asilimia 6.5 mnamo Juni 2023. Kiwango cha riba kwa mikopo ya siku kwa benki kilipanda hadi asilimia 7.2 kutoka asilimia 5.0. Mwezi Januari 2024, kamati ya sera ya fedha (MPC) ya benki kuu ilianza kutumia sera mpya ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ya Benki kuu (CBR). Riba hiyo iliongezwa hadi asilimia 6.0 mwezi Aprili 2024 kutoka asilimia 5.5 mwezi Januari 2024.

Viwango vya faida kwa mwaka huu hususani kwenye dhamana za serikali za muda mrefu ni zaidi ya viwango vilivyopatikana mwaka uliopita. Hata hivyo, ongezeko la faida kwenye uwekezaji wa dhamana hizo huleta matokeo chanya kwenye faida kwa wawekezaji.

### 4.7 Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni

Mnamo tarehe 30 Juni 2024, akiba ya fedha za kigeni ilifikia zaidi ya dola bilioni 5.0. Aidha, Benki kuu imekadiria akiba hiyo inatosha kukidhi mahitaji ya uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi kwa zaidi ya miezi minne. Dola moja ya Marekani iliuzwa shilingi 2,640.0 ikilinganishwa na shilingi 2,339.1 mnamo Juni 2023,

kwa kipindi cha mwaka mmoja shilingi ya Tanzania ilishuka thamani kwa asilimia 12.8 ikilinganishwa na asilimia 1.0 mwaka uliopita (Jedwali V). Benki kuu imechukua hatua kadhaa ikiwemo kuzuia utumiaji wa dola kwa mahitaji ya huduma na bidhaa zinazopatikana nchini. Hatua hizi zinatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni, kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya fedha ya Tanzania.

***Jedwali Na. V: Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni***

| Mwaka | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Viwango vya Kubadilisha Fedha | 2,264.1 | 2,300.9 | 2,307.9 | 2,310.4 | 2,315.7 | 2,339.1 | 2,640.0 |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

## 4.8 Soko la Mitaji na Dhamana

Kufikia tarehe 30 Juni 2024, ushiriki na uwekezaji kwenye soko la mitaji, dhamana na kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja uliongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja, benki mbili za biashara na shirika moja la serikali ziliorodhesha hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 482.4. Hatifungani hizo, ni kama ifuatavyo; Hatifungani ya Kijani ya muda wa miaka 5 kwa faida ya asilimia 10.25 ya benki ya CRDB, hatifungani ya maendeleo na ya kijamii ya miaka 3 kwa faida ya asilimia 9.5 ya benki ya NMB, pamoja na hatifungani ya Mamlaka ya maji TANGA kwa muda wa miaka 10 kwa faida ya asilimia 13.5 kwa mwaka.

Mifuko miwili ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka sokoni, kwani meneja aitwae Alpha Capital Ltd alizindua mfuko wa Alpha Halal na Zan Securities Ltd alizindua mfuko wa Timiza.

Hali ya ushiriki kwenye soko la mitaji, dhamana na uwekezaji kwenye mifuko ya pamoja nchini imeongezeka, ni matarajio yetu kuwa hali hii itazidi kuimarika na kuongezeka zaidi. Kuingia kwa wasimamizi wapya wa mifuko (meneja wa mifuko) ya uwekezaji wa pamoja na fursa zingine za uwekezaji sokoni ni ishara nzuri kwa UTT AMIS na soko kwa ujumla, na tunatarajia Taasisi au kampuni zingine kujiunga ili kuongeza ukwasi na ushindani jambo ambalo litaongeza zaidi ufanisi, faida na huduma bora.

### 4.8.1 Soko la Upili kwa Hatifungani na dhamana zilizoorodheshwa

Katika soko la upili, jumla ya thamani ya miamala ya dhamana za serikali za muda mrefu iliongezeka kwa shilingi trilioni 0.6 hadi kufikia shilingi trilioni 3.5 kutoka shilingi trilioni 2.9 mwaka uliopita. Thamani ya miamala ya hatifungani za kampuni binafsi zilizoorodheshwa ilikuwa shilingi bilioni 3.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.0 mwaka jana. Aidha, thamani ya miamala ya hatifungani za kampuni binafsi zilizoorodheshwa mwaka huu ni kubwa zaidi kwa shilingi bilioni 2.9 ikilinganishwa na mwaka jana. Ongezeko la thamani ya miamala limetokana na kuongezeka kwa hatifungani mpya zilizoorodheshwa sokoni.

### 4.8.2 Soko la Hisa

Mnamo tarehe 30 Juni 2024, thamani ya soko la Hisa la Dar es Salaam ni shillingi trilioni 16.8, ikiwa juu kwa asilimia 12.0 kutoka shillingi trilioni 15.0 mwaka jana. Asilimia ya ushiriki kwa wawekezaji wa ndani ni wastani wa asilimia 76.2, ikilinganishwa na asilimia 69.6 mwaka 2023. Pia, fahirisi ya Hisa kwa kampuni za ndani (TSI), iliongezeka kwa asilimia 9.3 hadi kufikia alama 4,475.2. Fahirisi ya kampuni zote sokoni (DSEI) iliongezeka kwa asilimia 12.0 hadi kufikia 2,016.9. Jumla ya mauzo ya soko katika kipindi hicho, iliongezeka kwa shilingi bilioni 165.0 hadi shilingi bilioni 272.6 kutoka shilingi bilioni 107.6 mwaka uliopita.

Katika kipindi hicho, baadhi ya kampuni zilitangaza na kulipa gawio kwa wanahisa. Gawio lililolipwa kwa kila hisa lilikuwa kama ifuatavyo; TCC - Sigara (Tsh. 500.0), TWIGA (TPCC) (Tsh. 390.0), TBL (Tsh. 537.0), NMB (Tsh. 361.18), SWISS (Tsh. 51.33), VODA (Tsh. 9.95), DSE (Tsh. 145.0) na CRDB (Tsh. 50.0).

### 4.8.3 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

Kwa kipindi cha mwaka mmoja kilichoishia tarehe 30 Juni 2024, idadi ya washiriki na rasilimali imeongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Aidha, jumla ya rasilimali zinazosimamiwa sokoni ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 1,550.7 hadi kufikia shilingi bilioni 2,273.6. Soko limetambulisha mifuko mipya miwili ambayo ni Alpha Halal na mfuko wa Timiza.

#### 4.8.3.1 Mifuko ya Uwekezaji ya UTT AMIS

Rasilimali za mifuko na huduma za uwekezaji zinazosimamiwa na UTT AMIS zimeongezeka kwa shilingi bilioni 702.8 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 538.9 lililonakiliwa mwaka jana. Aidha, rasilimali ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 1,535.4 hadi shilingi bilioni 2,238.2.

Mabadiliko chanya katika jumla ya rasilimali yanaonesha kuongezeka kwa imani ya wawekezaji katika bidhaa za UTT AMIS kutokana na usalama, faida shindani na urahisi wa kuingia na kutoka kwenye uwekezaji.

#### 4.8.3.2 Watumishi Housing Investments (WHI) – Faida Fund

Rasilimali za mfuko wa Faida zimeongezeka kwa shilingi bilioni 10.1 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 7.4 mwaka jana. Aidha,ukubwa wa mfuko umeongezeka kutoka shilingi bilioni 15.3 hadi shilingi bilioni 25.4. Thamani ya kipande mnamo Juni 2024 ilikuwa shilingi 115.8 ikilinganishwa na shilingi 104.9 Juni 2023.

#### 4.8.3.3 Zan Securities Limited (Zan) – Timiza Fund

Kulingana na waraka wa toleo la mfuko wa Timiza (offer document) unaonesha wawekezaji walianza kununua vipande kwa mara ya kwanza (mauzo ya awali) kwa bei ya shilingi 100.0 kwa kipande tarehe 27 Mei 2024 hadi tarehe 26 Juni 2024. Waraka huo unaonesha meneja alitarajia kukusanya rasilimali zenye thamani ya shilingi bilioni 10.0 sokoni.

***Vyanzo:*** *Benki kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, UTT AMIS, Watumishi Housing, Zan Securities Limited na Soko la hisa la Dar es Salaam.*

***Mwisho ninawatakia nyote msimu wa***
***sikukuu uliojaa furaha tele na heri ya mwaka mpya wa 2025***

***Wekeza Uwezeshwe!***

BOND FUND
More ideas for your money

# 9 Jarida la Habari

FUND
More ideas for your money

# Jarida la habari la UTT AMIS [Hadi tarehe 30 Septemba, 2024]

FUND
More ideas for your money

| 1.0 | **Maelezo Mafupi juu ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS** |
|---|---|
| | • Hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2024, Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS inasimamia jumla ya mifuko ya uwekezaji wa pamoja sita (6) ambayo ni : Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha,Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Jikimu, Mfuko wa Ukwasi na Mfuko wa Hatifungani.<br>• UTT AMIS inasimamia rasilimali zenye jumla ya thamani ya zaidi ya shilingi Trilioni 2.4<br>• Mwaka 2017 Kampuni ya UTT AMIS ilianzisha huduma ya usimamizi mali kwa kampuni na watu binafsi iitwayo UTT WEALTH MANAGEMENT yenye uwekezaji wenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 33.3.<br>• Wawekezaji ni zaidi ya **358,123**<br>• Mifuko hii ya uwekezaji wa pamoja hutoa faida shindani na ukwasi ukilinganisha na maeneo mengine linganifu sokoni. |
| **2.0** | **Taarifa za ujumla za Mifuko na huduma iliyoanzishwa na kusimamiwa na kampuni ya UTT AMIS** |

| NA | JINA LA MFUKO | MAELEZO |
|---|---|---|
| 2.1 | **Mfuko wa Umoja** | Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Mei, 2005. Mfuko huu unalenga zaidi wawekezaji wenye malengo ya muda wa kati na mrefu, jambo ambalo huwawezesha kupata muda wa kutosha kujiwekea akiba na kukuza mtaji wao. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana zilizoorodheshwa.<br><br>**Sifa za mfuko ni:**<br>• Vipande vinauzwa kwa thamani halisi [hakuna gharama za kujiunga].<br>• Wawekezaji ni watu binafsi, vikundi na Taasisi, unaruhusiwa katika mfuko huu.<br>• Kiwango cha chini cha kujiunga ni vipande 10 (sawa na shilingi 10,074.1 mnamo Septemba 2024).<br>• Gharama ya kujiondoa inayotozwa ni 1% ya thamani halisi ya kipande.<br>• Mauzo ya vipande hufanyika ndani ya siku 10 za kazi baada ya maombi kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS.<br>• Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji huo.<br>• Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha. |

***Jedwali Na. 01; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2024***

| Tangu Kuanzishwa [Mei,2005] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 15.1% | 13.8% | 16.2% | 12.9% | 11.3% |

***Chati Na. 01; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi tarehe 30 Septemba 2024***



## 2.2 Mfuko wa Wekeza Maisha

Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Mei, 2007. Mfuko huu unatoa faida za aina 2 ambazo ni, faida ya kukuza mtaji pamoja na faida ya bima. Katika Mfuko huu, zaidi ya asilimia 99.0 ya rasilimali huwekezwa na kiasi kilichobaki hupelekwa katika huduma za bima. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana.

**Sifa za mfuko;**

- Mfuko unaruhusu mwekezaji mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 55 kujiunga.
- Mfuko una aina mbili za mpango wa kuwekeza: (a) kuwekeza kwa awamu na (b) kuwekeza kwa mkupuo.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo [hakuna gharama za kujiunga].
- Kwa mpango wa kuweka kila mwezi, kiwango cha chini ni shilingi 8,340/= (ikiwa mwekezaji ana lengo la kufikia kiasi cha shilingi Milioni Moja kwa miaka 10).
- Faida za bima zinazopatikana ni: - bima ya maisha, bima ya ajali, bima ya ulemavu wa kudumu na gharama za mazishi.
- Mfuko unampa fursa mwekezaji kuwekeza kwa mpangilio maalumu, mathalani anaweza kuchagua kuchangia kwa mwezi, mara mbili kwa mwaka au mara moja kwa mwaka.
- Mfuko unampa fursa mwekezaji kupanga na kuchagua lengo na mpango wa uwekezaji atakaoutekeleza na kuutimiza ndani ya miaka 10.
- Mwekezaji akifariki mrithi au mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji.

***Jedwali Na. 02; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2024***

| Tangu Kuanzishwa [Mei,2007] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 13.8% | 23.3% | 25.5% | 14.6% | 13.1% |

***Chati Na. 02; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi tarehe 30 Septemba 2024***



Watoto Fund

Faraja kwa Watoto

## 2.3 Mfuko wa Watoto

Mfuko ulianzishwa tarehe 01 Oktoba 2008. Mfuko una lengo la kuwanufaisha watoto kwa kujiwekea akiba na kutumia uwekezaji wao kukidhi gharama za shule na kupata mtaji kwa maendeleo ya baadae. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana.

**Sifa za Mfuko;**

- Uwekezaji ni kwa ajili ya mtoto mwenye umri chini ya miaka 18.
- Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi 10,000/= na kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi 5,000/= na kuendelea.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo. [ hakuna gharama za kujiunga ]
- Mfuko unatoa Mpango wa kukuza mtaji.
- Mzazi au Mlezi ataruhusiwa kuuza au kupunguza sehemu ya uwekezaji wake pindi mtoto atakapofikisha umri wa miaka 12.
- Taasisi, kampuni na vikundi vinaweza kuwawekezea watoto kama sehemu ya huduma kwa jamii

***Jedwali Na. 03; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2024***

| Tangu Kuanzishwa [Okt,2008] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 12.9% | 16.1% | 19.9% | 14.8% | 14.5% |

***Chati Na. 03; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi tarehe 30 Septemba 2024***



| | | |
|---|---|---|
| 2.4 | **Mfuko wa Jikimu** | Mfuko ulianzishwa tarehe 03 Novemba 2008. Lengo la mfuko ni kuwawezesha wawekezaji kupata gawio kutokana na mapato ya ziada katika vipindi tofauti na kukuza mtaji kwa mwekezaji wa muda mrefu. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana. |

**Sifa za Mfuko:**

Aina ya mpango wa uwekezaji

- (a) Mpango wa kukuza mtaji ni kuanzia shilingi. 5,000/= (b) Mpango wa kupata gawio kila robo mwaka (Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi milioni 2) na (c) Mpango wa kupata gawio kwa mwaka (kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi milioni 1).
- Kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi 5,000/= kwa mpango wa kukuza mtaji na shilingi 15,000/= kwa mpango wa kupata gawio.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo [ hakuna gharama za kujiunga]
- Mfuko unatoza gharama za kujitoa kama ifuatavyo: (a) 2.0% kwa mwekezaji aliedumu ndani ya mfuko kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja. (b) 1.5% kwa mwekezaji aliedumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya mwaka 1 na chini ya miaka 2. (c) 1% kwa uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya miaka 2 na chini ya miaka 3 na, (d) Uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya miaka 3 hakuna gharama za kujitoa.
- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji (ndani ya siku 10 za kazi baada ya maombi ya kuuza vipande kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji.

***Jedwali Na. 04; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2024***

| Tangu Kuanzishwa [Nov, 2008] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| **16.1%** | 16.5% | 15.6% | 14.9% | 14.6% |

***Jedwali Na. 05; Gawio kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2024***

| Taarifa | Shilingi Bilioni | Kwa kila kipande, shilingi |
|---|---|---|
| Tangu Kuanzishwa [Nov, 2008] | 16.9 | 185.5 |
| Mwaka Mmoja [Okt 23-Sept 24] | 1.0 | 12.0 |

***Chati Na. 04; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi tarehe 30 Septemba 2024***



2.5

**Mfuko Wa Ukwasi (Liquid Fund)**

Mfuko ulianzishwa tarehe 01 Machi, 2013. Ni Mfuko wa wazi ambao unatoa fursa kwa wawekezaji wenye lengo la muda mfupi, wa kati na mrefu. Ni mfuko wa wazi ambao rasilimali zake huwekezwa katika maeneo yenye vipato vya kudumu (fixed income instruments).

**Sifa za mfuko:**

- Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi 100,000/= na kiwango cha nyongeza kisichopungua shilingi 10,000/=.
- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha zake za mauzo ya vipande, (ndani ya siku 3 za kazi baada ya maombi ya kuuza vipande kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS)
- Mfuko hauna gharama yoyote ya kujiunga wala kujitoa.
- Mfuko unaruhusu watu binafsi,vikundi au Taasisi kuwekeza.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo (hakuna gharama za kujiunga).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili anaruhusiwa kuendeleza uwekezaji.

***Jedwali Na. 06; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2024***

| Tangu Kuanzishwa [Machi, 2013] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 13.2% | 13.6% | 13.9% | 13.4% | 13.0% |

***Chati Na. 05; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi tarehe 30 Septemba 2024***



**BOND FUND**
*More ideas for your money*

**2.6** — **Mfuko wa Hatifungani (Bond Fund)**

Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Septemba, 2019. Ni mfuko wa wazi ambao rasilimali zake huwekezwa katika maeneo yenye vipato vya kudumu (fixed income instruments). Mfuko una lengo la kutoa gawio, kulingana na faida itakayopatikana na kukuza mtaji kwa wawekezaji wa muda mrefu.

**Sifa za mfuko:**

Kuna aina tatu za mpango wa uwekezaji katika Mfuko huu:

- Mpango wa kukuza mtaji
- Mpango wa gawio kila mwezi na
- Mpango wa gawio kila baada ya miezi sita.

Kiwango cha chini cha kuanza kuweketa.

(a) Shilingi 50,000 kwa mpango wa kukuza mtaji

(b) Shilingi milioni 10 kwa mpango wa gawio kila mwezi na

(c) Shilingi milioni 5 kwa mpango wa gawio kila baada ya miezi sita.

- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji, (ndani ya siku 10 za kazi baada ya kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili anaruhusiwa kuendeleza uwekezaji.

***Jedwali Na. 07; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2024***

| Tangu Kuanzishwa [Sept,2019] | Miaka 3 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|
| 14.5% | 13.0% | 12.3% | 12.4% |

***Jedwali Na. 08; Gawio kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2024***

| Taarifa | Shilingi Bilioni | Kwa kila kipande, shilingi |
|---|---|---|
| Tangu Kuanzishwa [Sept,2019] | 69.2 | 57.0 |
| Mwaka Mmoja [Okt 23 - Sept 24] | 30.1 | 12.0 |

***Chati Na. 06; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi tarehe 30 Septemba 2024***




| 2.7 | **Huduma ya usimamizi mali / UTT Wealth Management** | Huduma hii ilianzishwa mnamo mwaka 2017, kwa kuweka kipaumbele malengo ya kifedha ya watu binafsi, familia, vikundi na Taasisi za ndani na nje ya nchi. Huduma hii hutengeneza uwekezaji kulingana na mahitaji na malengo ya mwekezaji. |
|---|---|---|

**Sifa za huduma hii:**

- Kiwango cha chini cha kuwekeza ni shilingi milioni 100 na kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi Milioni 10.
- Huduma hii inampa fursa mwekezaji kuwekeza kwenye uwekezaji wa muda mrefu sokoni huku akipata nafasi ya kuongeza au kuuza sehemu ya uwekezaji wake kulingana na hali ya soko.
- Katika kufanikisha huduma hii mwekezaji atalipia asilimia 1.0 kwa mwaka kama gharama ya usimamizi wa rasilimali zake.
- Uwekezaji katika huduma hii, unatoa fursa kwa wawekezaji kuchagua mpango wa kupata malipo ya faida kila baada ya miezi 6 na mpango wa kukuza mtaji.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji

***Chati Na. 05; Mwenendo wa Rasilimali kwa Huduma ya Usimamizi Mali tarehe 30 Septemba 2024***




## 3.0 Elimu kwa Wawekezaji

More ideas for your money

| 3.1 | **Unawezaje kujiunga na Mifuko ya UTT AMIS?** | Mtanzania mkazi na asiye mkazi, mtu binafsi, Taasisi, vikundi wawekezaji wawili (Jointly) wanaruhusiwa ku wekeza katika Mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS. Jinsi ya kuwekeza : |
|---|---|---|

- Mwekezaji binafsi anaweza kujiunga kwa kubonyeza *150*82# na kujisajili kwenye programu tumizi (UTT AMIS APP) ambayo inaweza kupakuliwa kwenye 'App Store' au 'PlayStore'
- Mwekezaji anatakiwa kujaza fomu ya kufungua akaunti kwa ajili ya kukamilisha usajili (KYC FORM).
- Kikundi na Taasisi, wawekezaji wawili (Joint) atajaza fomu ya kufungua akaunti ya UTT AMIS pamoja na viambatanisho vinavyotambulika kisheria (Certificate of Registration,Muhtsari wa Kikao, NIDA za Watia saini n.k) na kuvituma kupitia barua-pepe uwekezaji@uttamis.co.tz au kuleta kwenye Ofisi za UTT AMIS zilizo karibu nawe au Tawi lolote la CRDB au Madalali wote walioidhinishwa na Soko la Hisa la Dar es salaam. Kwa wawekezaji walio nje ya nchi, kwa akaunti ya mtu binafsi au watu wawili watajaza fomu ya kufungua akaunti na kisha kuambatanisha kitambulisho cha uraia.
- Baada ya kupata akaunti namba ya Mfuko uliouchagua na kukamilisha taratibu zote za usajili (KYC Form) mwekezaji anaweza kuanza na kuendelea kuwekeza kupitia njia za simu kama vile TigoPesa, Mpesa, AirtelMoney, Halopesa. T-Pesa, Azam Pesa na Ezypesa au njia za kibenki kupitia CRDB, NMB, NBC na STANBIC.

3.2 **Nini maana ya kiwango cha Mfumuko wa bei? Na jinsi gani inamuathiri mwekezaji?**

Kwa tafsiri rahisi, mfumuko wa bei ni alama inayotafsiri mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa kipindi fulani sokoni. Kuongezeka kwa kiwango cha mfumuko wa bei huashiria kupungua kwa thamani ya fedha au kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma sokoni.

Kuna sababu nyingi za kiuchumi zinazopelekea kutokea kwa hali hii, hususani ongezeko la fedha katika mzunguko kusikoendana na kasi ya ukuaji wa uchumi na hivyo matokeo yake kupelekea mfumuko wa bei.

Kiujumla, vigezo vilivyokubalika kupima viwango vya mfumuko wa bei ni pamoja na Bei za bidhaa za Jumla (Wholesale Price Index)], Bei za mahitaji ya kawaida ya walaji (Consumer Price Index), Mabadiliko ya pato la ndani la nchi (GDP) n.k . Vile vile, Bei za mahitaji ya kawaida ya walaji (Consumer Price Index) inapima gharama za bidhaa mbalimbali za msingi zinazotumiwa na kundi la watu ikiwakilisha makundi yote ya jamii kama kigezo cha upimaji wa uchumi katika nchi.

Ni muhimu kutambua kuwa, kazi ya kuangalia hali ya mfumuko wa bei katika nchi hufanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Jambo la msingi la kujifunza ni kuwa, Katika uchumi wenye mfumuko wa bei, unashauriwa kuwekeza mara kwa mara hata kama kiasi cha kuwekeza ni kidogo. Kwa kujenga nidhamu hio, unaweza usione madhara au athari hasi za kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika uwekezaji.

3.3 **Nini maana ya Faida Jumuishi?**

Kwa ufupi, ni faida inayopatikana kutoka katika uwekezaji ambao hugeuzwa mtaji na hivyo kutoa faida kubwa zaidi hapo baadae tofauti na uwekezaji wa muda maalum ambao faida inayopatikana inatokana tu na muda uliokaa ndani ya uwekezaji.

Je utajali ikiwa utapata faida ya asilimia 10 au 12 katika uwekezaji?

Ukweli ni kuwa, ukizingatia hilo utaweza kutengeneza tofauti kubwa katika ukuaji wa faida na mtaji kadiri muda unavyoenda/unavyoongezeka. Faida itokanayo na kompaundi inatokana na faida kuendelea kuongeza mtaji ambao huleta mapato makubwa kila mwaka. Mapato makubwa au faida kubwa au uwekezaji wa muda mrefu inaongeza kiasi cha mtaji kwa uwiano wa kijiometri.

**Matokeo ya Faida jumuishi.**

Kwa kutumia jedwali hapo chini, unaweza kuona matokeo ya nguvu ya kompaundi na faida zake kutokana na uwekezaji uliofanywa mara moja kwa kiasi cha shilingi 50,000/= na 5,000,000/= katika vipindi mbalimbali na kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 09;**

| Faida | 12% | | 14% | |
|---|---|---|---|---|
| Mwaka/Kiasi | 50,000/= | 5,000,000/= | 50,000/= | 5,000,000/= |
| 1 | 56,000.00 | 5,600,000.00 | 57,000.00 | 5,700,000.00 |
| 3 | 70,246.40 | 7,024,640.00 | 74,077.20 | 7,407,720.00 |
| 5 | 88,117.08 | 8,811,708.42 | 96,270.73 | 9,627,072.91 |
| 10 | 155,292.41 | 15,529,241.04 | 185,361.07 | 18,536,106.57 |
| 20 | 482,314.65 | 48,231,465.47 | 687,174.49 | 68,717,449.36 |

Jedwali namba 10, linaonesha matokeo ya nguvu ya kompaundi kutokana na faida zake kwa uwekezaji uliofanywa mara moja kwa kiasi cha shilingi milioni hamsini (50) na shilingi milioni mia moja (100) katika vipindi mbalimbali na kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 10;**

| Faida | 12% | | 14% | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka/ Kiasi** | **50,000,000/=** | **100,000,000/=** | **50,000,000/=** | **100,000,000/=** |
| 1 | 56,000,000.00 | 112,000,000.00 | 57,000,000.00 | 114,000,000.00 |
| 3 | 70,246,400.00 | 140,492,800.00 | 74,077,200.00 | 148,154,400.00 |
| 5 | 88,117,084.16 | 176,234,168.32 | 96,270,729.12 | 192,541,458.24 |
| 10 | 155,292,410.42 | 310,584,820.83 | 185,361,065.71 | 370,722,131.41 |
| 20 | 482,314,654.66 | 964,629,309.33 | 687,174,493.59 | 1,374,348,987.19 |

Nguvu ya kompaundi na faida yake inaoneshwa kwenye majedwali yafuatayo kwa mwekezaji anaewekeza kiasi cha shilingi 50,000/=, 100,000/=, 500,000/=, na shilingi milioni 1 kwa kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 11;** Uwekezaji wa shilingi 50,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 628,278.40 | 634,125.15 | 640,037.27 |
| 36 | 3 | 2,089,091.05 | 2,153,843.92 | 2,221,139.98 |
| 60 | 5 | 3,871,853.61 | 4,083,483.49 | 4,309,756.26 |
| 120 | 10 | 10,242,248.95 | 11,501,934.47 | 12,953,445.60 |
| 240 | 20 | 37,968,441.80 | 49,462,768.27 | 65,058,300.25 |

BOND FUND
More ideas for your money

**Jedwali Na. 12;** Uwekezaji wa shilingi 100,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 1,256,556.81 | 1,268,250.30 | 1,280,074.54 |
| 36 | 3 | 4,178,182.11 | 4,307,687.84 | 4,442,279.95 |
| 60 | 5 | 7,743,707.22 | 8,166,966.99 | 8,619,512.51 |
| 120 | 10 | 20,484,497.89 | 23,003,868.95 | 25,906,891.21 |
| 240 | 20 | 75,936,883.60 | 98,925,536.54 | 130,116,600.51 |

**Jedwali Na. 13;** Uwekezaji wa shilingi 500,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 6,282,784.05 | 6,341,251.51 | 6,400,372.68 |
| 36 | 3 | 20,890,910.55 | 21,538,439.18 | 22,211,399.75 |
| 60 | 5 | 38,718,536.09 | 40,834,834.93 | 43,097,562.55 |
| 120 | 10 | 102,422,489.45 | 115,019,344.73 | 129,534,456.05 |
| 240 | 20 | 379,684,417.99 | 494,627,682.69 | 650,583,002.53 |

**Jedwali Na. 14;** Uwekezaji wa shilingi 1,000,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 12,565,568.09 | 12,682,503.01 | 12,800,745.36 |
| 36 | 3 | 41,781,821.09 | 43,076,878.36 | 44,422,799.50 |
| 60 | 5 | 77,437,072.17 | 81,669,669.86 | 86,195,125.10 |
| 120 | 10 | 204,844,978.90 | 230,038,689.46 | 259,068,912.10 |
| 240 | 20 | 759,368,835.99 | 989,255,365.39 | 1,301,166,005.06 |

Kutokana na jedwali hapo juu, utagundua kuwa sio busara kupoteza muda na pesa. Inabidi utambue kuwa, MUDA ni kigezo muhimu katika kufanya maajabu ya kompaundi.

**Jambo la msingi la kujifunza:**

(1) Wakati wote, tumia fursa zilizopo katika uwekezaji kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni; usalama, ukwasi pamoja na kiwango cha faida.

(2) Endelea kuwekeza kwa muda mrefu ili unufaike na maajabu ya kompaundi.

## 4.0 Mawasiliano

Kwa maelezo zaidi kuhusu Mifuko yetu, tafadhali wasiliana nasi kwa anuani zifuatayo:

**Ofisi ya UTT DAR ES SALAAM**
Ofisi za UTT AMIS Dar es Salaam
Afisa Mtendaji Mkuu,
UTT AMIS Plc,
Ghorofa ya Pili (2), Jengo la Sukari, Mtaa wa Sokoine Drive na Ohio,
S.L.P 14825, Dar es Salaam
Simu Namba: +255 (0) 22 2128460
Namba za Bure: 0800112020
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz
Tovuti: www.uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MBEYA**
Ghorofa ya Pili, Jengo la NHIF, Mbeya
S.L.P 1210, Mbeya,
Simu Namba: +255 (0) 25 2500371
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MWANZA**
Mezzanine, Jengo la NSSF Commercial Complex
S.L.P 640, Mwanza,
Simu Namba: +255 (0) 28 2505072
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS DODOMA**
Ghorofa ya Sita, Jengo la PSSSF,
Mtaa wa Makole,
S.L.P 1310, Dodoma
Simu Namba: +255 (0) 26 2323861
Nukushi: +255 26 2323862
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ARUSHA**
Ghorofa ya Nne, Jengo la Ngorongoro Conservation,
S.L.P 2490, Arusha,
Simu Namba: +255 (0) 27 2970625
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ZANZIBAR**
Ghorofa ya Tatu, Jengo la Sheikh Thabit Kombo- Michenzani
S.L.P 2190, Zanzibar
Simu Namba: +255 (0) 24 2941274
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

BOND FUND
More ideas for your money

BOND FUND

*More ideas for your money*

## Mifuko Mingine ya Uwekezaji ya UTT AMIS

UMOJA FUND

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

Jikimu Income Scheme
Live Well ...You Deserve It

UKWASI FUND
Uhuru kwa mwekezaj

Wekeza Maisha
Invest Life